SportPesa

CHEZA USHINDE SASA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

**Machinga wapewa siku tatu kuhuma, watengewa maeneo mapya**



UKURASA 2




Jumapili Oktoba 31, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580750

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

RIPOTI MAALUM

## Huu ndio 'uchafu' madereva malori

**Mwandishi** asafiri nao Shinyanga-Dodoma saa 18, ashuhudia yaliyojificha...*Endelea ukurasa 4*



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Wilbroad Mutafungwa.



Rais Samia Suluhu Hassan, akisindikizwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kushoto) na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akiondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, kwenda Glasgow, Scotland kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa (UN) utakaojadili athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na jitihada za kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa ili kupunguza joto Duniani. **PICHA: IKULU.**

## Udanganyifu waponza mamia mtihani la VII

UKURASA 2

## Operesheni usalimishaji silaha nchini yatangazwa

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, COASTAL MECHI YA REKODI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Machinga wapewa siku tatu kuhama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ametoa siku tatu kwa wafanyabiashara ndogo, maarufu machinga, kuhamia katika maeneo yaliyotengwa kulingana na bidhaa wanazouza.

Vilevile, ametangaza eneo la Engutoto lililoko Kata ya Engutoto litumike kwa muda kwa malori kupakua na kupakiza mizigo wakati wakitafuta maeneo mengine kwa ajili ya shughuli hizo.

Mongela alitoa agizo hilo jana eneo la Kilombero jijini Arusha alipozungumza na machinga, akiambatana na viongozi wa wafanyabiashara hao na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Alisema kuwa hadi kufikia Novemba 3 mwaka huu, wafanyabiashara hao wawe wameshahamia kwenye maeneo hayo yaliyotengwa ambayo ni Soko la Kilombero likalokuwa linauza mboga, matunda na bidhaa za chakula.

Alisema Soko la Mbauda litakuwa na bidhaa zote za mitumba, Soko la Ulezi litauza nguo za dukani, Machame Luxury vifaa vya eletroniki pamoja vifaa vya nyumbani, Soko la Engutoto vifaa vya kuchomelea, vitanda, makochi na vitu vingine vinavyohusiana na bidhaa hizo huku Soko la Kwamrombo likitumika kwa ajili ya minada ya nguo na nyinginezo.

"Hatukatai changamoto tupeane taarifa ili tuzitate, sisi sio malaika ni binadamu yawezekana katika zoezi hili tukaghafirika, basi tushauriane na namshukuru Mwenyekiti wa Machinga Mkoa wa Arusha, Aminah Njoka na timu yake kwa ushauri wao tunashirikiana, tuendelee kushirikiana," alisema.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara wenye uwezo, wakafanye biashara katika maeneo yao waliopangiwa na sio maeneo ya machinga ambao wanalipa Sh. 20,000 kwa mwaka.

Alionya asitokee machinga akakimbilia eneo ambalo hajapangwa kwa kuwa kila eneo lina mpangilio wake na utaratibu utakuwapo chini ya usimamizi wa Jiji la Arusha kupitia kwa Mkurugenzi wa Jiji hilo, Dk. John Pima na wataalamu wake.

Mwenyekiti wa Machinga, Aminah, alisifu uamuzi wa Rais Samia Hassan Suluhu wa kuagiza wafanyabiashara hao wapangwe.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kulia), akiteta jambo na Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Lebaratus Sabas katika kikao na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, wakati akitoa siku 30 kwa wamiliki haramu wa silaha kuzisalimisha katika vituo vya polisi, ofisi za Serikali za Mitaa na kwa Watendaji wa Kata. **PICHA: WMNN**

# Udanganyifu waponza mamia matokeo la VII

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani (NECTA) limetangaza matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka huu, watahiniwa 393 wakifutiwa matokeo yao baada ya kubainika kufanya udanganyifu.

Akitangaza matokeo hayo jana mkoani Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alisema matokeo hayo yamefutwa kwa sababu watahiniwa walibainika kuingia ndani ya chumba cha mtihani na vitu visivyotakiwa.

Dk. Msonde alisema baraza limezishauri mamlaka zinazohusika, kuwachukulia hatua kwa mujibu wa kanuni za utumishi na sheria, wale wote waliohusika kwa namna moja ama nyingine kusababisha kutokea kwa udanganyifu.

"Makosa yao yamejikita zaidi kwa watahiniwa kuyatenda wenyewe kwa wenyewe kwa kuingia na vitu visivyotakiwa ndani ya chumba cha mtihani zikiwamo notsi, kubadilishana karatasi za majibu na kuigiliziana, kuwa na mfanano wa majibu usio wa kawaida.

"NECTA imezuia matokeo ya watahiniwa 128 ambao waliugua au kupata matatizo na kushindwa kufanya mtihani huo na watahiniwa wamepewa fursa ya kuufanya tena mwaka 2022," alisema.

Kuhusu mtihani huo, alisema jumla ya watahiniwa 1,132,084 wa shule za msingi walisajiliwa, wasichana wakiwa ni 584,614 (asilimia 51.64) na wavulana 547,470 (asilimia 48.36).

Alisema watahiniwa wenye uhitaji maalum walikuwa ni 3,238, sawa na asilimia 0.29.

"Watahiniwa 1,108,023, sawa na asilimia 97.87 ya waliosajiliwa waliufanya na kati yao wasichana ni 574,998 (asilimia 98.36) na wavulana ni 533,025 (asilimia 97.36).

Alisema watahiniwa 24,061, sawa na asilimia 2.13, hawakufanya mtihani kwa sababu mbalimbali zikiwamo utoro na ugonjwa na kati yao, wasichana ni 9,616 na wavulana ni 14,445.

"Ufaulu wa jumla unaonyesha watahiniwa 907,802 kati ya 1,107,460, wasichana wakiwa ni 574,704 na wavulana ni 532,756 waliotunukiwa matokeo wamefaulu.

"Idadi hii ya watahiniwa waliofaulu ni sawa na asilimia 81.97, kati yao wasichana ni 467,967 (asilimia 81.43) na wavulana ni 439,835 (asilimia 82.56). Mwaka 2020 idadi ya watahiniwa waliofaulu ilikuwa 833.672 hivyo, idadi ya watahiniwa waliofaulu mwaka 2021 imeongezeka kwa watahiniwa 74,130, sawa na asilimia 8.89 kulinganishwa na mwaka 2020," alisema.

**10 BORA KITAIFA**

Eluleki Haule (St. Anne Marie, Dar), Happy Deus (Twibhoki, Mara), John Charles, Twibhoki, Mara), Joshua Jacob (Twibhoki, Mara), Eva Chengula (Fountain of Joy, Dar), Joctan Matara (Twibhoki, Mara), Barnaba Magoto (Twibhoki, Mara), Rahma Juma (Mtuki Highland, Dar), Juliana Shimbala (St. Joseph's, Dar) na Jackline Mtewele (Masaka, Dar).

**WASICHANA 10 BORA KITAIFA**

Happy Deus (Twibhoki, Mara), Eva Chengula (Fountain of Joy, Dar), Rahma Juma (Mtuki Highland, Dar), Juliana Shimbala (St. Joseph's, Dar), Jackline Mtewele (Masaka, Dar), Irene Lucas (St. Peter Claver, Kagera), Veronica Kakwezi (Twibhoki, Mara), Paulyn Mayengo (Fountain of Joy, Dar), Faith Masanja (Mzigu, Mwanza) na Mage Gweya (Viczone, Mara).

**WAVULANA 10 BORA KITAIFA**

Eluleki Haule (St. Anne Marie, Dar), John Charles (Twibhoki, Mara), Joshua Jacob (Twibhoki, Mara), Joctam Matara (Twibhoki, Mara), Barnaba Magoto (Twibhoki, Mara), Dominic Mwita (Graiyaki, Mara) Gabriel Ndagije (Twibhoki, Mara), James Marwa (Twibhoki, Mara) John Mgonja (Decent (Dar) na Kilugala Ngala (Kwema Modern, Shinyanga).

**SHULE 10 BORA**

Dk. Msonde alitaja shule 10 bora kitaifa kuwa ni Graiyaki (Mara), St. Peter Claver (Kagera), Rocken Hill (Shinyanga), Kemebos (Kagera), Bishop Caeser (Kagera), Kwema Modern (Shinyanga), St. Magret (Arusha), Waja Springs (Geita), Kadama (Geita na Chalinze Modern Islamic (Pwani).

Dk. Msonde alitaja mikoa 10 iliyoongoza kitaifa kuwa ni Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Arusha, Njombe, Kilimanjaro, Katavi, Lindi, Simiyu na Pwani.

"Halmashauri na manispaa 10 zilizoongoza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Liwale, Uvinza, Butiama, Mtama, Musoma, Chemba, Kasulu (TC), Hanang, Bahi na Kondoa TC," alisema.

Dk. Msonde alisema matokeo yanaonyesha ufaulu wa watahiniwa katika masomo ya Hisabati, Kiswahili, Sayansi na Teknolojia, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi na Uraia na Maadili upo juu ya wastani isipokuwa somo la Kiingereza ambalo ufaulu wake upo chini ya wastani.

Alisema baraza litafanya uchambuzi wake wa kina katika matokeo hayo kwa kila somo na kutoa machapisho yatakayowasilishwa kwa wadau wa elimu zikiwamo shule.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya St. Anne Marie, Gradius Ndyetabula, alisema: "Shule hii ina miaka 22 tangu kuanzishwa kwake, tumekuwa tukitoa wanafunzi 10 bora lakini kumpata mwanafunzi bora kwa kwanza kitaifa hii ni mara ya kwanza na inatokana na uwekezaji uliofanywa kwenye miundombinu na ukomavu wa shule," alisema.

# HABARI KITAIFA

## Mabeyo ataka ubunifu JKT

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, ameliagiza Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuendelea kubuni miradi ya maendeleo nchini.

Jenerali Mabeyo alitoa agizo hilo jana alipozindua kituo cha burudani cha Medeli East ambacho kitakuwa na ukumbi mkubwa, eneo la huduma ya chakula na michezo ya watoto.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa jeshi hilo, hivyo ni vema wakaendelea kuwa wabunifu ili kuzidi kujitegemea.

"Tusiendelee kulalamika tu, fursa zipo tuzitafute tuzitengeneze, zinaweza kujitokeza lakini ukisubiri fursa zitengenezwe na mwingine wewe ukazichukue, unakuwa mhalifu na mhalifu kila siku utakuwa unafukuzwa,"alisema.

Jenerali Mabeyo alisema wameanza na miradi midogo ndani ya vikosi vya jeshi lakini watakuwa na miradi mikubwa, akisisitiza majeshi mengi duniani yameendelea kutokana na ubunifu.

Alisema kituo hicho cha burudani kinapaswa kutunzwa ili kushindana kibiashara.

"Huduma bora pekee yake ndio zitakazosaidia kupata wateja wa kutosha. Kama huduma zenu zikiwa ovyo ovyo, watu watakimbia, wataenda sehemu nyingine," alisema.

Mkuu wa Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema ukumbi huo wenye uwezo wa kuchukua watu kati ya 1,000 na 1,200 kwa wakati mmoja, una maeneo mengine ya kumbi ndogo, jengo la utawala, ukumbi wa watu maarufu, eneo la huduma ya chakula na eneo la michezo kwa watoto.

Alisema ukumbi huo utatumika kwa shughuli za kijeshi na za kijamii.

## Makandarasi wanawake wakumbukwa kwa miradi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema serikali itatenga miradi maalum ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ambayo itatekelezwa na makandarasi wanawake ili kuwajengea uwezo na uzoefu wa kufanya kazi katika miradi mikubwa.

Alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam alipozindua Chama cha Makandarasi Wanawake (TWCA) kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema dhamira ya serikali ni kuona makandarasi wazawa wanafanya kazi katika miradi mbalimbali ikiwamo ya kimkakati ili kusaidia kasi ya ukuaji wa uchumi.

Prof. Mbarawa alisema kuwa kupitia TWCA, wanaamini watazalishwa wataalamu mahiri na wenye uzoefu wa kufanya kazi kwa pamoja na kuleta tija kwa maendeleo ya sekta ya ujenzi.

Waziri huyo pia alizitaka wizara na taasisi za serikali kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na kanuni zake, kutoa kipaumbele kwa makundi maalum hasa kundi la makandarasi wanawake kwa kupata kazi ndogo na kubwa za miradi inayoendelea kutekelezwa.

Rais wa TWCA, Judith Odunga, alisema makandarasi wanawake wamekuwa wakikabiliwa na matatizo ya kutopewa miradi mikubwa ya kiwango cha lami kutokana na ukosefu wa mitambo.

"Tunaomba wizara yako iangalie namna ya kutudhamini kwa kampuni zenye mitambo ili zitukopeshe mitambo na Wizara ya Ujenzi itupatie miradi maalum mikubwa ya kiwango cha lami na madaraja makubwa kwa ajili ya kutujengea uwezo," alisema.

Mlezi wa chama hicho, Rais Mstaafu wa Kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika, Getrude Mongela, alisema anatamani kuona mabilionea wakizalishwa kutoka katika sekta hiyo na kuwataka makandarasi hao kushika miradi mikubwa.




Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo (wa pili kulia), akifungua pazia kuzindua ukumbi wa burudani wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), uliopo Medeli East, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Operesheni usalimishaji wa silaha yatangazwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ametangaza operesheni ya usalimishaji silaha haramu kwa hiari nchi nzima itakayoanza kutekelezwa kesho hadi Novemba 30, mwaka huu.

Amesema atakayeshindwa kutumia muda huo wa neema, atachukuliwa kama mtuhumiwa wa uhalifu.

Kupitia tangazo la Serikali Na. 774 la Oktoba 29, mwaka huu, waziri huyo amesema ametangaza msamaha wa kutowashtaki wale wote watakaosalimisha silaha kwa hiari kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa kwenye tangazo hilo.

Simbachawene alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipotoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu tangazo la msamaha na usalimishaji wa silaha kwa wamiliki wa silaha kinyume cha sheria.

"Silaha hizo zisalimishwe katika vituo vyote vya Jeshi la Polisi nchini na ofisi za serikali za mitaa na kwa watendaji wa kata kuanzia muda wa saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni," alisema.

Alibainisha kuwa nchi nyingi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) ikiwamo Tanzania, zimetia saini na kuridhia mikataba, itifaki, maazimio na makubaliano mbalimbali ya kuzuia uzagaaji wa silaha ndogo na nyepesi.

Waziri huyo alisema kuwa moja ya makubaliano hayo ya Julai 2018 kuhusu udhibiti wa uzagaaji wa silaha haramu.

"Uzaagaji wa silaha haramu duniani umekuwa ukisababisha uvunjifu wa amani na ukosefu wa usalama na kusababisha hofu kwa watu, vifo na majeruhi," alisema.

Alionya kuwa baada ya muda huo wa neema kupita, msako mkali utafanyika nchi nzima ili kuwakamata wote walioikaidi nafasi ya msamaha waliyopewa.

"Zoezi hili litakuwa ni kwa mwezi Novemba tu na yeyote atakayeshindwa kusalimisha silaha ndani ya muda uliotamkwa, atachukuliwa kama mtuhumiwa kulingana na sheria, kanuni na taratibu za nchi.

"Ninatoa wito kwa wananchi wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria, kuhakikisha wanatekeleza ipasavyo zoezi, pia nawasisitiza wananchi ambao ndugu zao walikuwa wamiliki silaha kihalali na sasa wamefariki dunia, kuhakikisha wanazisalimisha silaha hizo kulingana na masharti niliyoyataja," alisema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ILALA

Kitongoji UKONGA Mkoa D'SALAAM

Shauri la Madai Na. 175/2017

MDAI DAVID NYAMBEHO ELIAS

MDAIWA TUJIJENGE TZ LTD

KIITWA SHAURINI MDAIWA

Kwa: DAVID NYAMBEHO ELIAS

PUGU

FIKA KUTEKELEZA HUKUMU

25/11/2021 saa 8:30

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
UKONGA WILAYA YA ILALA

(Sahihi ya Mdaiwa)

(Sahihi ya Mwenye Kutoa Shauri)

216546702

IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
FOR MARA
AT MUSOMA

APPLICATION No. 125 OF 2021

1. TUJIJENGE TANZANIA LIMITED
2. NYABWEKA METRIDA KWAM ..................... APPLICANTS

VERSUS

NICKSON . K. ELIAKIMU ......................RESPONDENT

**SUMMONS/NOTICE**

TO,
**NICKSON K. ELIAKIMU**

The above mentioned applicant has instituted a suit at this Court, against you, particulars of which are mentioned in a copy of application which is obtainable from the registry of this Court, **YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS COURT** in persons(s) or by recognized agent(s) for mention on 19th November, 2021 at 08:00am in the fore noon.

**TAKE NOTICE THAT;**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence

Given under my hand and seal of this Tribunal this 26th day of October, 2021.

Kitungulu, E
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara

216546702

RIPOTI MAALUM

# Mapenzi yalivyo kichaka cha ajali za barabarani

## ■Ushuhuda 'uchafu' wa dereva kazini
## ■Mkuu Trafiki: Ni kweli, tunapambana

**Na Lawrence Matongo,**
SHINYANGA

NI saa 12 asubuhi, jua likiashiria mawio, kukiwa na baridi kali, safari ya kwenda mjini Dodoma kwa lori inaanza eneo la Ibinzamata mjini Shinyanga.

Kwa lugha rahisi ya mazungumzo, hiyo ni safari ya wastani wa saa saba na nusu kwa anayetumia basi, umbali wa Km 536.5.

Maelewano ya nauli na utingo wa lori hilo ni Sh. 15,000, ikiambatana na masharti ya kukaa kwenye kitanda kilichopo nyuma ya dereva na hairuhusiwi kuingia eneo hilo ukiwa umevaa viatu.

Dereva Maganga (siyo jina lake halisi), akionekana mwenye mwili uliojengeka kwa mazoezi na lishe, anaingia ndani ya gari kutekeleza majukumu yake, huku akihakikishiwa na utingo wake kwamba 'kila kitu kiko sawa'.

Mara moja Nipashe kupitia udadisi wake kwa utingo, inabaini lori hilo lenye wastani wa kubeba mizigo tani 10, lina shehena ya mahindi kutoka wilayani Misungwi mkoani Mwanza, ilikochukuliwa mchana siku iliyopita na kuwasili mjini Shinyanga usiku.

Baada ya kulala mjini hapo, asubuhi siku inayofuata wenye gari wakaanza tena safari na abiria huyo mpya kuelekea mjini Dodoma.

Ndani ya dakika 45, dereva anasimamisha gari kwa mapumziko kwenye mji mdogo wa Tinde, wastani wa takriban Km 34, wote waliomo kwenye lori hilo wanashuka ili kupata kifungua kinywa.

Baada ya dakika 28 kituoni hapo, dereva anaelekeza safari iendelee na inatekelezwa kwa mwelekeo wa barabara hiyo kuu ya lami inayogota jijini Dar es Saalam.

Kilomita chache kabla ya kuingia mjini Nzega (Km 37 kutoka Tinde), dereva anapunguza mwendo na kusimama, akitoa lugha ya udhuru kwa abiria wake "nisubirini kidogo nikapunguze uzito".

Nipashe inaachwa njiapanda na msamiati huo, hata kuamua kusaka tafsiri kutoka kwa mwenyeji wake utingo, ambaye hapindishi sentensi, akitamka: "Mke wake yuko Dar, hapa ana 'mchepuko' tu".

Ndani ya mapumziko hayo ya lazima takriban saa moja, dereva anatokea na mara moja safari inaendelea hadi mjini Singida.

Hata hivyo, Nipashe inashuhudia mengi zaidi ya ilichodokezwa, safari hii njiani kabla ya kufika Singida, kukiwapo vituo kadhaa anakosimamisha gari, naye akianika ukweli kwa utambulisho "shemeji yenu" maeneo ya Igunga na Shelui, akiwataja majina yao.

Saa 10 jioni, wakiwa mjini Singida, dereva anamwagiza utingo wake anunue jogoo kwa ajili ya chakula cha jioni na baada ya saa tano, yaani saa tatu usiku, anapaki gari na kulikabidhi kwa mlinzi kwenye maegesho rasmi, jirani na Stendi ya Mabasi Manyoni.

Baada ya hapo, anamgeukia utingo na abiria, akiwaelekeza: "Tutapumzika hapa (Manyoni) kwa leo, saa kumi na moja na nusu (11:30) alfajiri tuwe hapa" kisha anakabidhi jogoo kwa 'shemeji yenu' aliyefika kumlaki.

Unapotimu muda elekezi, safari ya kwenda mjini Dodoma inaendelea, lakini saa mbili baadaye, majira ya saa 1:30 asubuhi, dereva anaomba udhuru alale walau kwa saa moja kwenye kitanda cha lori hilo.

Hiyo ni baada ya kunusurika kugongana uso kwa uso na lori lingine linalotoka mjini Dodoma, dereva anakiri sababu kuu ni kuelemewa na usingizi.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Wilbroad.

Baada ya mapumziko hayo, safari inaendelea hadi majira ya saa sita mchana mzigo unaposhushwa, huku abiria akiagana nao.

**SHIDA ILIKOJIFICHA**

Ushuhuda wa Nipashe mara moja unabaini kuwapo uhusiano mkubwa kati ya uzembe wa madereva na uendekezaji ngono dhidi ya usalama wa malori ya masafa marefu.

Kilichojiri kwenye safari hiyo iliyopaswa kuchukua muda wa saa saba na nusu, lakini ikachukua siku moja na nusu, kinatoa ujumbe wa tatizo kubwa la nidhamu ya madereva.

Ni hoja ambayo Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa, anakiri imo kwenye orodha ya sababu kuu zinazochangia ajali za barabarani.

Kamanda Mutafungwa anafafanua kuwapo ukiukwaji wa sheria, baadhi ya madereva wa malori na utingo wao kwa makusudi wanapakia abiria na marafiki zao wa kike, hivyo kuongeza matukio ya ajali yasiyokoma.

Ikirejewa Kifungu cha 58(II) cha Sheria ya Usalama Barabarani iliyopo nchini sasa, kinapiga marufuku magari ya mizigo kupakia abiria na kinaelekeza adhabu za kuchukuliwa.

Kamanda Mutafungwa pia anataja vyanzo vingine vya ajali walivyovibaini kutoka kwa dereva ni: Uchovu, matumizi ya vilevi na kutokuzingatia tahadhari za usalama barabarani, ikiwamo ishara za dharura.

Eneo lingine analolianisha ni kwamba majira ya alfajiri yana ajali nyingi, nusu yake zikisababisha vifo na majeruhi.

"Pamoja na kuwapo kwa utingo ndani ya gari, bado wanapakia abiria kinyume cha taratibu. Abiria aliyepakiwa na utingo ndiyo waathiriwa wakuu wa ajali.

"Baadhi ya madereva, siyo wote, ajali hizi kuna uhusiano mkubwa na tabia ya ulevi," anaeleza.

"Madereva wengi nyakati za usiku, akisimama sehemu kupumzika, anaingia kwenye starehe baa kisha asubuhi anarudi kwenye usukani," anafafanua.

Anarejea takwimu za Jeshi la Polisi zilizoandaliwa kwa kipindi mahususi cha miezi minne kati ya Januari na Aprili kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita kwenye Barabara ya Morogoro, zinaonesha athari kubwa.

Kamanda Mutafungwa anaainisha, mchanganuo kwamba kati ya malori ya mizigo 843 yaliyofanyiwa utafiti, 546 yalipata ajali na kusababisha vifo vya watu 466 na majeruhi walikuwa 489.

Kimsingi, takwimu hizo zina maana kwamba asilimia 65 (theluthi mbili) ya malori hayo yaliyopita kwenye barabara hiyo yalipata ajali.

Pia ni inatoa taswira ya wastani wa vifo vya watu 45 kila mwezi, sawa na vifo vya watu 11 kila wiki.

Upande wa majeruhi, inamaanisha kuna watu 60 wanaojeruhiwa kila mwezi, sawa na watu wawili kwa siku.

**JICHO LA POLISI**

Kamanda Mutafungwa anataja hatua wanazoendelea kuzichukua ni pamoja na kujikita katika utoaji elimu kwa madereva na wadau wengine wa barabara.

Anabainisha kwamba ajali hizo kwa kiwango kikubwa hutokea usiku wa manani au alfajiri, kutokana na uchovu wa madereva, unaochangiwa na wamiliki wa malori kutoajiri madereva wawili wa kupokezana.

Uainishaji wake kitaalamu ni kwamba kila baada ya saa nane, dereva anapaswa kupokewa na mwenzake, kwa sababu kiafya anakuwa hayuko vyema kumudu jukumu hilo.

"Alfajiri kunapopambazuka kawaida mtu akipigwa na kiubaridi anasinzia. Dereva huyu aliyechoka atalala muda huu," anafafanua.

Kuhusu hatua wanazochukua, anasema wanaendesha oparesheni za kudhibiti ajali, akiwa na angalizo la adhabu kwa wanaokiuka sheria, mahakamani kuna faini ya hadi Sh. 150,000 au kifungo cha mwaka mmoja gerezani au adhabu zote mbili kwa pamoja.

**TAKWIMU AJALI ZA MALORI**

| Mwaka | Ajali | Vifo | Majeruhi |
|---|---|---|---|
| 2019 | 331 | 272 | 271 |
| 2020 | 159 | 147 | 152 |
| 2021 | 56 | 47 | 66 |

***Hali ya ajali za barabarani zilizohusisha malori kwa kipindi cha miezi minne ya mwanzo (Januari hadi Aprili) kwa miaka mitatu mfululizo nchini.*** CHANZO: Kikosi cha Usalama Barabarani.

**UFAFANUZI KITABIBU**

Daktari wa Magonjwa ya Dharura katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Biita Muhanuzi, ana ufafanuzi wa athari hizo za ajali, kama alivyohojiwa na Nipashe katika mazungumzo yafuatayo:

**SWALI:** Kitalamu mtu anapaswa kulala kwa muda gani (idadi ya saa) kwa siku ili awe na afya bora?

**DAKTARI:** Ili uwe na afya bora, kitabibu unatakiwa uwe unapata usingizi walau kwa saa nane kwa siku.

**SWALI:** Mtu asipopata usingizi wa kutosha, anapata athari zipi kiafya?

**DAKTARI:** Anakuwa kwenye hatari ya kupata 'stress' (sonona), kusinzia akiwa kazini, kushindwa kufanya kazi vizuri na kuwa na uchovu.

**SWALI:** Mtu asiyepata usingizi wa kutosha, anaathirika vipi katika utendaji wake wa kazi?

**DAKTARI:** Hawezi kufanya kazi vizuri, anawahi kuchoka na ufanisi wake wa kazi unapungua.

**SWALI:** Vipi kuhusu madereva wa masafa marefu?

**DAKTARI:** Madhara ndiyo hayo yanayolalamikia kila siku - kusababisha ajali na hata kupoteza maisha.

## HABARI KITAIFA

# Waiangukia serikali athari madini risasi

**Na Romana Mallya**

ASASI isiyo ya kiserikali ya AGENDA imeishauri serikali na wadau wengine kuongeza ushirikiano katika juhudi za kuondoa rangi zenye madini ya risasi nchini kwa sababu yanasababisha matatizo mbalimbali ikiwamo katika via vya uzazi, upungufu wa damu, figo na ini.

Ofisa Programu Mkuu wa AGENDA, Silvani Mng'anya, alipaza kilio chao hicho juzi mkoani Dar es Salaam walipoungana na asasi 49 kutoka nchi 36 ambazo ni wanachama wa mtandao wa kimataifa wa IPEN katika kuhamasisha suala hilo.

Alisema wanashiriki maadhimisho ya wiki ya kimataifa ya kuzuia madhara hayo ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni "Kushirikiana kwa pamoja ili kuwa na dunia isiyo na rangi zenye madini ya risasi".

Ofisa huyo alisema rangi zenye madini ya risasi pia husababisha shinikizo la juu la damu na matatizo ya kinga ya mwili.

"Madhara ya rangi zenye madini ya risasi yanaweza kuwa makubwa na kudumu na yasiyotibika hasa kwa watoto wadogo chini ya miaka sita," alisema.

Ofisa Programu Mwandamizi wa AGENDA, Dorah Swai, alisema Tanzania kupitia Shirika la Viwango (TBS), ilishaweka kiwango cha madini ya risasi katika rangi mwaka 2017 ambacho ni sehemu ya 90 kwa milioni.

"Hii inamaanisha kiasi hiki cha madini zinazoingizwa, zinazozalishwa, zinazosambazwa na kuuzwa hazitakiwi kuzidi kiwango hicho.

"Kwa sasa kuna kiwango kimoja kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Tanzania ni kati ya asilimia 43 ya nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO) zenye udhibiti wa kisheria kwa mujibu wa taarifa ya Agosti 31, mwaka huu ya WHO, hili ni ongezeko kutoka asilimia 39 mwezi Mei 2020," alisema.

Katibu Mtendaji wa asasi hiyo, Haji Rehani, alisema uelewa wa jamii kuhusu suala hili ni jambo la msingi ili kuhakikisha watumiaji wanaepuka kununua na kutumia rangi ambazo hazijakidhi kiwango cha TBS.

# 'Taasisi ziajiri wenye taaluma'

**Na Halifan Chusi**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, amezitaka taasisi nchini kuajiri maofisa mawasiliano na uhusiano waliosomea taaluma hiyo ili kuepuka makosa yanayofanywa na baadhi ya maofisa uhusiano wasio na taaluma hiyo.

Dk. Jim Yonazi alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na wadau mbalimbali wakati wa mkutano mkuu wa Chama cha Maofisa Uhusiano kwa Umma Tanzania (PRST) uliofanyika Dar es Salaam.

Mkutano huo uliandaliwa na PRST kwa lengo la kujadili masuala mtambuka ya kitaaluma.

Dk. Yonazi alisema serikali inatambua juhudi ambazo zinafanywa na vyama vya kitaaluma ikiwamo PRST na kuahidi kuwapa ushirikiano kuhakikisha taaluma hiyo inajengwa na kulindwa kwa wivu mkubwa.

"Niseme tu serikali itakuwa bega kwa bega na ninyi na hapa nilipo, viongozi wenzangu wizarani wanajua nipo hapa kwa ajili ya kushirikiana na ninyi katika mkutano huu," alisema.

Rais wa PRST, Rothi Makuza, alisema lengo la mkutano huo ni kutathmini majukumu halisi ya maofisa uhusiano kwa kile alichodai kuwa kinafanywa na maofisa uhusiano wengine sio kile kinachopaswa kufanyika.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile, alibainisha kuwapo vikwazo kwa baadhi ya maofisa habari pindi wanahabari wanapohitaji taarifa, hivyo kuomba PRST kulitazama vizuri suala hilo.

# Maelfu kunufaika mradi wa maji

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wa Kijiji cha Saranga, Wilaya ya Babati mkoani Manyara wamekabidhiwa mradi wa maji safi wenye gharama ya Sh. milioni 422 unaotarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wakazi 2,500 wa eneo hilo.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la WaterAid, Anna Mzinga, alibainisha faida za mradi huo alipoukabidhi kwa wanakijiji hao, ukijengwa kwa ufadhili wa WaterAid kwa kushirikiana na Coca-Cola Foundation na People Pstcode Loter.

Alisema mradi huo ambao ni wa awamu ya pili wa kuwapatia wananchi maji safi na salama, umetekelezwa kwa miezi 11 kuanzia Oktoba 2020.

"Tumekuwa mashahidi wa namna mabadiliko ya tabianchi yalivyoleta athari katika ukanda wa Afrika Mshariki, Tanzania ikiwamo, kusababisha ukame, mafuriko na ukosefu wa majisafi na salama kutokana na kukauka kwa vyanzo vya maji," alisema.

Mzinga alisema WaterAid inasherehekea manufaa ya mradi endelevu wa maji vijijini unaowezesha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali za Maji kutoka Wizara ya Maji, Pamella Temu, alisema maeneo yao mengi bado hayana vyanzo vya maji vya uhakika.

"Kwa hapa Manyara, tunafurahi tumepata maji kwa kuchimba visima, kuteka chemchemi na hata kuvuna mvua, lakini bado tuna matatizo kadhaa katika vyanzo hivi, uharibifu wa vyanzo vya maji unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo mvua kubwa au ndogo katika vipindi visivyotarajiwa, mafuriko na kiangazi kikali," alisema.


# NOTISI/ TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | MICHAEL GROUP LIMITED | 1.BRC MAKING MACHINE QTY:1<br>2.WELDED MESH MAKING MACHINE QTY:2<br>3.ATOMATIC WIRE DRAWING MAKING MACHINE QTY:5 | MICHAEL GROUP LTD | KINYEREZI | 23/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | TEMSO ENGINEERING & CONSTRUCTION COMPANY LTD | 1.NYUMBA,HATI NAMBA 58326<br>2.GARI T.430 CMY- DAF TRACTOR<br>3.GARI T.825 ATE- MITSUBISHI FUSO<br>4.GARI T.646 CPA- TRAILER<br>5.GARI T.280 AYM- TRAILER<br>6.HYDROLIC SWING MACHINE QC12Y163200,2010<br>7.MECHANICAL SHEERING MACHINE<br>8.HYDRAULIC BENDING MACHINE,WC 67Y2010<br>9.GRADING MACHINE<br>10.PRESSING MACHINE,HEVY DUTY,QTY:2<br>11.PRESSING MACHINE,SMALL SIZE,QTY:3<br>12.ROLLING MACHINE<br>13.UNIVERSAL MILLING MACHINE<br>14.PRESSING MACHINE MEDIUM SIZE<br>15.LATHE MACHINE,QTY:3<br>16.BENDING MACHINE,UK<br>17.SAND FABRIC MACHINE<br>18.HYDRAULIC POWER MACHINE<br>19.DRILLING MACHINE<br>20.WELDING MACHINE<br>21.POTTEL WELDING MACHINE<br>22.WELDING MACHINE 250<br>23.SAW MACHINE COMPLETE WITH MOTOR | RAYMOND LUDOVICK TENGA<br><br>TEMSO ENGINEERING CONSTRUCTION CO.LTD | NYUMBA-PUGU KAJIUNGENI<br>MAGARI-CHANIKA<br>MASHINE-SIDO VINGUNGUTI | NYUMBA NI TAREHE 24/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA<br>MAGARI,TAREHE 18/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA<br>MASHINE,TAREHE 19/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | HASSAN BUGANGA KAPOJONGO | NYUMBA | HASSAN BUGANGA KAPOJONGO | USTAWI-BUZURUGA | 17/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | FAISAL SALUM HASSAN | GARI T396 DJR HINO RAINBOW | FAISAL SALUM HASSAN | TEMEKE | 24/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | RANGE DANIEL ROTENTE | KIWANJA NA NYUMBA | NASHON RANGE ROTENTE NA RANGE DANIEL ROTENTE | KIWANJA-PUGU MWAKANGA NA NYUMBA-MBONDOLE | 25/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | HELENA ANTONY HALENGO | NYUMBA | MARIA ANTONY SKAWEWE | MAPELELE-ILEMI | 17/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | HALENGO-NZOVWE | 18/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | JOHN MARTINI LUGOME | NYUMBA MBILI | JOHN MARTINI LUGOME | ILEMI | 22/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | ANDERSON MITAMBO SANGA | NYUMBA | FELISTER KLEMENT MAMBOLEO | ILOMBA | 25/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | DEOGRAS LUCAS KAPESA | NYUMBA | DEOGRAS LUCAS KAPESA | MJI MWEMA-SONGWE | 26/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | FELIX MAVIKE MSIGWA | NYUMBA | FELIX MAVIKE MSIGWA | ILEMI | 19/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | TIMOTH JULIUS MANYANGU | NYUMBA | HARUNI MICHAEL MHAVILE | CHIMALA | 17/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | RICHARD APOLINARY MHIMBIRA | NYUMBA | RICHARD APOLINARY MHIMBIRA | ILOMBA | 29/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | ENGELIBAERT ANDREA MALLYA | NYUMBA | ISSA AMBILIKILE MWANDUHA | SONGWE | 26/11/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

## MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba ,kiwanja,Gari au Mashine papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0754497396/ 0784252048/ 0652691275/ 0743885084/ 0678799566/ 0718038313
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216546602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi kupunguza muda vibali vya mazingira ni mwafaka kwa maendeleo

**KWA** muda mrefu kumekuwa na malalamiko juu ya upatikanaji wa vibali vya tathmini ya athari za mazingira (EIA) kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

Katika malalamiko hayo, baadhi ya makandarasi wamekuwa wakidai kuwa baada ya kutuma maombi, mhusika anatakiwa kusubiri takribani siku 105 ndipo apate kibali, jambo ambalo limekuwa likisababisha kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika ripoti yake ya mwaka 2019/20, alidokeza umangimeza huo akiweka bayana kuwa suala hilo huchukua muda mrefu kukamilika. Kwa mujibu wa CAG, hadi kupata kibali hicho ni wastani wa siku 95.

Licha ya kusubiri kwa muda mrefu, imekuwa ikidaiwa kuwa mwombaji pia anatakiwa kugharamia kikao cha kujadili maombi pamoja na kuwalipa posho wajumbe, jambo ambalo linaibua ukakasi na kuwapo kwa mazingira ya rushwa.

Kwa mantiki hiyo, mwombaji anaweza kutumia gharama kubwa katika kufuatilia kibali ikiwamo kuwapo kwa mazingira ya kufanyika vikao viwili au zaidi mpaka kufikia hatua ya upatikanaji wake.

Hata hivyo, matumaini yameanza kuonekana baada ya serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuagiza kwamba muda huo upunguzwe kutoka siku 105 hadi 14 hadi 30.

Mwanga wa kupatikana kwa ufumbuzi wa kero hiyo, umeonekana baada ya kikao cha pamoja kati ya Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo na Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Hassan Chande. Viongozi hao walikutana juzi kujadili suala hilo ili kupata ufumbuzi wa kucheleweshwa kwa vibali, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli katika muda uliopangwa.

Bila kuuma maneno, viongozi hao walibainisha kwamba kuchelewa kwa upatikanaji wa vibali hivyo, kumekuwa kikwazo katika miradi mingi. Hatua hiyo ilitokana na ukwamishaji wa vibali vya tathmini ya athari za mazingira katika ujenzi wa minara ya mawasiliano.

Katika kutatua kero hiyo, mawaziri hao waliagiza wataalamu wa wizara yenye dhamana ya mazingira pamoja na zile zinazosimamia miradi ya maendeleo kama mawasiliano na ujenzi, kuunganisha mifumo yao ili kuondoa visingizio vya kutopatikana vibali kwa wakati.

Ili kuhakikisha suala hilo linatekelezwa, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliahidi kufanya kazi na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambao ndio chanzo cha malalamiko kutokana na ucheleweshaji wa vibali kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano. Mkurugenzi huyo pia aliahidi kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na viongozi hao, ikiwamo kupatikana kwa vibali ndani ya siku siku 14 mpaka 30.

Uamuzi huo wa kupunguza muda wa kutoa vibali kutoka NEMC ni wa kupongezwa kwa kuwa utaondoa malalamiko ya miaka mingi juu ya urasimu uliokuwapo. Licha ya urasimu pia utapunguza mazingira ya rushwa kutoka kwa baadhi ya watendaji wa NEMC kwa kuwa kuwapo kwa muda mrefu kunatia ushawishi wa waombaji kutoa rushwa ili kupatiwa huduma hiyo.

Pamoja na kupunguzwa kwa muda huo, pia ni vyema suala la kuwabana waombaji wa vibali kugharimia vikao pamoja na kuwalipa posho wajumbe liangaliwe upya kwa kuwa nalo lina ukakasi ndani yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa nini kuna mizengwe mikopo asilimia 10 kwa makundi haya?

**HALMASHAURI** nchini, zimekuwa zikitoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi matatu ambayo ni ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ili yafanye biashara mbalimbali kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Utoaji wa mikopo hiyo ni kutekeleza agizo la serikali la mwaka 1998 linalozitaka halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya makundi hayo.

Vilevile, viongozi wa serikali wamekuwa wakiyahimiza makundi hayo kuchangamkia fursa hiyo ya mikopo, kwa kuwa hatua hiyo kutenga asilimia 10, inalenga kuharakisha ukuaji wa uchumi mpana.

Uchumi mpana na jumuishi unakusudia kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa na kunufaisha watu wengi kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji mali na hivyo kusaidia makundi hayo kunufaika na mikopo hiyo.

Katika kiasi hicho cha asilimia 10 kinachotengwa na kila halmashauri, wanawake na vijana wao kila kundi limetengewa asilimia nne, huku watu wenye walemavu wakiwa wametengewa asilimia mbili.

Pamoja na kuwapo kwa fungu hilo, kwa ajili ya makundi hayo, inaelezwa kuwa kumekuwapo na urasimu katika kupata mikopo hiyo kwenye baadhi ya halmashauri, hali inayochangia kuwakatisha tamaa walengwa.

Ni katika kongamano la kujadili vikwazo vinavyowakabili watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, lililofanyika juzi jijini Dar es Salaam linaibuliwa hilo na baadhi ya washiriki wa kongamano hilo.

Mbele ya Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Dar es Salaam, Judith Kimaro, inaelezwa kuwa baadhi ya wanawake wamekata tamaa baada ya safari za nenda rudi za kufuatilia mikopo bila mafanikio.

Wanawake hao ambao ni wazazi wa watoto wenye ulemavu huo, wanajiweka katika kundi la walemavu kwa vile ni walezi wa watoto hao, ambapo

**Ni katika kongamano la kujadili vikwazo vinavyowakabili watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, lililofanyika juzi jijini Dar es Salaam linaibuliwa hilo na baadhi ya washiriki wa kongamano hilo.**

wanahitaji mikopo wafanye biashara, ili walee vizuri watoto wao.

Wanabainisha kuwa kuna urasimu wa kupata mikopo hiyo licha ya kufuata taratibu zote zinazotakiwa, ikiwamo kusajili vikundi kuwa na akaunti benki, bado wengi wao hasa wanaolea walemavu hao, hawajafanikiwa.

Kwa ujumla ni kwamba, yapo mengi ambayo wanawake hao walilalamikia kwenye kongamano hilo kuhusu urasimu wanaokumbana nao wanapohitaji mikopo kutoka kwenye halmashauri.

Hata hivyo, Ofisa Ustawi wa Jamii, Judith Kimaro, anawataka waendelee kufuatilia, na siyo lazima wawe katika vikundi, bali siku hizi utaratibu umebadilika, na kwamba hata mtu mmoja anaweza kukopeshwa. Kwa mtazamo wangu ni kwamba, kama malalamiko hayo yana ukweli ndani yake, ni vyema waliopewa jukumu la kusimamia mikopo hiyo wakaangalia uwezekano wa kumaliza kikwazo hicho.

Ninaamini kwamba, utoaji wa mikopo hiyo unasaidia kuharakisha ukuaji wa uchumi mpana na jumuishi wenye kupunguza umaskini katika jamii na hata kunufaisha watu wengi kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji mali.

Kwa kuwa maofisa maendeleo ya jamii wana jukumu la kusajili vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kuratibu mikopo ya vikundi hivyo, ingekuwa vyema kama watasikia malalamiko hayo.

Lakini pia, wakati mwingine, inawezekana zikawapo sababu za msingi zinazochangia baadhi ya watu kunyimwa mikopo, kama vile kukosa uaminifu hali ambayo inaweza kuzifanya halmashauri kuwanyima.

Kama hakuna tatizo, ni vyema wanawake, vijana na walemavu wakakopeshwa, ili wafanye biashaara walizokusudia na kurejesha mikopo kwa wakati ili watu wengine waweze kukopeshwa.

Iwapo bado kuna ukosefu wa elimu, basi ni vyema wahusika waelimishwe zaidi kwa ajili ya kufuata utaratibu wote unaotakiwa, ili mwisho wa siku wapate mikopo hiyo wajikwamue kiuchumi.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Ni wakati mwafaka sasa serikali kuunga mkono juhudi za AZAKI



Na Pascal Mayalla

**Kwa wiki nzima iliyopita tumeshuhudia Wiki ya AZAKI ikirindima jijini Dodoma. Mimi na kampuni yangu ya PPR, tulikuwa wadau wakuu wa Wiki ya AZAKI.**

SI mara moja wala mbili katika safu hii, nimekuwa nikizungumzia hoja ya Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe na misaada kutoka kwa wafadhili, itumike tu kama mitaji. Ni ukweli usiopingika kwamba maendeleo ya kweli ni yale yanayotoka ndani na si ya kuletewa na watu wa nje.

Moja ya makala hizo ni ile ya Septemba 5, 2021, isemayo "Serikali Iunge Mkono Juhudi za TradeMark East Africa (TMEA) katika kuleta Maendeleo. TMEA inafadhiliwa ni mashirika ya nchi wafadhili wa ughaibuni na ndio wamejenga vituo vyote vya ushuru wa pamoja katika mipaka yote ya nchi za Afrika Mashariki.

Septemba 12, 2021 pia niliandika "Juhudi za TWCC, Kuwainua Wanawake, Ziungwe Mkono". Taasisi hizo zote mbili ni asasi za kiraia (AZAKI) na zinafanya mambo makubwa kwa ufadhili wa watu wa nje.

Kwa wiki nzima iliyopita tumeshuhudia Wiki ya AZAKI ikirindima jijini Dodoma. Mimi na kampuni yangu ya PPR, tulikuwa wadau wakuu wa Wiki ya AZAKI. Jukumu langu lilikuwa kutangaza kila kilichojiri katika wiki hiyo, toka siku ya uzinduzi mgeni rasmi akiwa Spika wa Bunge, Job Ndugai na kufungwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima.

Katika hotuba yake kuzindua wiki hii, Spika Ndugai alizitaka AZAKI kutumia utafiti na takwimu vizuri vitakavyosaidia kutoa majawabu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii ya Watanzania.

Alisema asasi hizo hazina budi kutafuta fedha ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuleta tija na vipaumbele vya taifa. Hii maana yake jukumu la kutafuta fedha limeachwa kwa AZAKI zenyewe, wakati kiukweli, shughuli nyingi zinazofanywa na baadhi ya asasi hizo ni zile ambazo zingepaswa kufanywa na serikali. AZAKI zinafanya kazi bega kwa bega kusaidia kuleta maendeleo Tanzania, hivyo serikali ina wajibu wa kuzisaidia na si kuendelea kuziacha zikitegemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje ya nchi.

Moja ya vitu vizuri Spika Ndugai aliponifurahisha ni pale alipozishauri AZAKI kufanya kazi kwa weledi, uadilifu na uzalendo kwa maslahi mapana ya taifa. Ukumbi mzima ulimshangilia pale alipozipasha AZAKI bila kupepesa macho kwa kuzitaka kuendelea kuikosoa serikali na viongozi wake lakini pia zina wajibu wa kuwapongeza pale wanapofanya vizuri, wanapotekeleza majukumu yao kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wote. Alisema haiwezekani kila siku ni kukosoa tu lakini kwenye mazuri, unakaa kimya.

Hili jambo la ukosoaji Spika alilolizungumza ni jambo zuri lenye afya na manufaa makubwa kwa maslahi kwa taifa. Hakuna binadamu yeyote aliye mkamilifu, hivyo viongozi nao ni binadamu. Wanaweza kukosea, wakosolewe kwa heshima, lugha ya staha na ukosoaji huo ufanyike kwa nia njema na si kubeza, kubagaza, kukebehi, kuzodoa, bali kukosoa kwa nia ya kujenga. Hata kwenye mazuri, pongezi zitolewe.

Japo siungi mkono Spika kutumia jukwaa la AZAKI, kupiga kijembe cha mtu kuitwa zuzu, kwa maoni yangu, kama kuna mtu yoyote anawaita wenzake mazuzu, mtu huyo akabiliwe na kutakiwa kuthibitisha huo uzuzu wale anaowaita hivyo. Ni ukweli usiopingika kuwa binadamu hatufanani, kuna wengine ni wazuri na kuna wengine kweli ni mazuzu.

Ikitokea mtu amemwita mtu mwingine zuzu, mwita zuzu akabiliwe athibitishe huo uzuzu anaousema kuwaita wenzake mazuzu. Akishindwa kuthibitisha, achukuliwe hatua. Lakini kiukeli kuna mazuzu miongoni mwetu, dawa ni kujitathmini na kujitafakari tukaondokana na uzuzu.

Rais wa Taasisi ya Uwezeshaji Asasi za Kiraia (Foundation for Civil Society- FCS) Dk. Stigmata Tenga, alisema iko haja kwa Bunge kuleta mabadiliko na kupitia upya sheria, taratibu na miongozo ambayo inaziongoza asasi hizo ili zishiriki vyema katika kutekeleza kazi zao na majukumu yao kwa maendeleo ya taifa.

**255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Vijana wa Kitanzania kuna leo na kesho



Na Joseph Kulangwa

**Hivi sasa baada ya hukumu ya Mahakama Kuu inayomtaka kulipa mabilioni ya fedha; kuwalipa Benard Membe, Fatma Karume na Profesa Anna Tibaijuka, wako washangiliaji lakini wako pia wanaomhurumia.**

USEMI maarufu wa hujafa hujaumbika una maana kubwa sana kwamba umuhimu wa mtu hujibainisha pale anapokuwa ameaga dunia. Hapo ndipo utasikia sifa kedekede kwamba alikuwa hivi, alikuwa vile.

Kabla hujafa, huwezi kusikia sifa hizo ingawa zingine huwa hasi na zingine chanya. Lakini ukiwa hai watakaa nazo kimya wakisubiri siku yako ya kufarakana na dunia yako na kwenda kuanza maisha mapya ahera.

Binadamu duniani tumegawanyika katika makundi mawili, yenye hisia na misimamo tofauti, kuhusu maisha na kuhusu watu waishio duniani ndiyo maana wewe ukimpenda fulani huyu atamchukia.

Mmoja anaweza kushangaa kwa nini huyu anampenda yule, hali kadhalika huyu naye atamshangaa kwa nini yule anampenda huyu. Hii ni mitazamo na imani walizo nazo binadamu kuhusu mambo, vitu na watu.

Lakini tunajifunza hapa hapa kambi hizo mbili na hakuna anayeweza kumshurutisha huyu kuamini au kupenda lile. Ni matakwa binafsi yatokanayo na faragha ya kila mtu na kadri aaminivyo.

Tunayaona yakijitokeza, mfano mzuri ni wa hivi karibuni, kumhusu 'Mwanaharakati Huru', ndugu yangu Cyprian Musiba, ambaye yamemkuta mahakamani kutokana na kauli zake alizopata kutoa siku za nyuma.

Wako watu walizipenda na kuzishabikia bila kujali athari hasi zilizokuwa zikiwapata aliowashambulia. Lakini pia wako waliokuwa wakizifurahia na kuzishangilia na kuziona ndizo zenyewe hasa. Wakiziona chanya.

Alionekana katika tasnia ya habari kama shujaa kwa waliokuwa wanamkubali na kauli zake, akitamba kumtetea Rais John Magufuli na kujiapiza kuwa yu tayari kufa, ikawa kama tamthiliya maarufu za Ertugrul na Sultani ambako askari hujiapisha kupoteza maisha kwa ajili ya Sultani na Bey.

Hivi sasa baada ya hukumu ya Mahakama Kuu inayomtaka kulipa mabilioni ya fedha; kuwalipa Benard Membe, Fatma Karume na Profesa Anna Tibaijuka, wako washangiliaji lakini wako pia wanaomhurumia.

Mabilioni hayo ni mengi kwa kijana kama huyu kuweza kuyalipa huku akijulikana kutokuwa na ukwasi wa aina hiyo. Nini kinafuata? Bila shaka katika taratibu za kimahakama zinazowapa walalamikaji fursa ya kukazia hukumu, ni majanga.

Hivi sasa wameibuka waliodai kuchafuliwa naye wakiwamo Nape Nnauye, Yusufu Makamba na Zitto Kabwe. Pamoja na kumshukuru Mungu kwa uamuzi wa Mahakama, sasa wanataka waliokuwa nyuma ya Musiba waibuke waseme nao ni upi upande wao.

Ni yale yale ya mwana umleavyo ndivyo akuavyo. Musiba alilelewa hivyo- kuchafua watu kulikothibitishwa na Mahakama ambako hakukukemewa enzi hizo, pengine angeacha na kuwapa uhuru wa kupumua aliokuwa akiwananga na kuwachafua!

He, kumbe ni yale yale kama ya Lengai ole Sabaya, ambaye tayari ni mfungwa baada ya Mahakama kukubaliana na upande wa Jamhuri kuwa alichokifanya akiwa Disii wa Hai hakikustahili, hivyo kustahili tu kifungo cha miaka 30 gerezani.

Haya yote yaliyotokea kupitia mahakama zetu nchini, bila shaka yanatufungua macho kuona ni nini kibaya kinachoweza kuzuiwa na kusikia, ni nini kibaya kinachoweza kuachwa kuzungumzwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Watanzania tunaweza kujifunza kupitia matukio haya pengine na mengine ambayo yako njiani kuibuka katika mahakama hizi hizi. Tena bahati mbaya sana, yanafanywa au yakifanywa na vijana na wakalindana mpaka sasa walikuwa na hatamu, ndio sasa mahakama zimewashushia marungu.

Kama Sabaya na Musiba wangezingatia kuwa kuna leo na kesho, wakaona umuhimu wa utawala bora na kuuheshimu, leo tusingekuwa tunashangilia au kusikitika kwa yaliyoamuliwa na Mahakama.

Je, sasa waliokuwa nyuma ya vijana wetu hawa, wako tayari kutoka mbele na kutoa ushuhuda wao na hata kuomba radhi kwa kuwasukuma kufanya waliyofanya na kuumiza watu kimwili na kiakili?

Kama wako tayari hawajachelewa na ndiyo sababu wanaombwa kusimama hadharani na kuuambia umma wa Watanzania waliokuwa wakiumia kupitia kauli za Mwanaharakati Huru na vitendo vya Jenerali Sabaya. Tunashindwa nini? Mbona majirani Rwanda walifanikiwa kupitia Gacaca? Watamke neno ili wasamehewe duniani na ahera, kwa kuwa hujafa hujaumbika!

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Hongera RC Mtaka kwa kuzuia mil.47/- posho ziara ya mafunzo



Na Thobias Mwanakatwe

**Baada ya RC Dodoma kuzuia fedha hizo kwenda kwenye mafunzo, mjadala mkali uliibuka kwenye mitandao ya kijamii baadhi wakifagilia hatua hiyo na wengine wakipinga wakitaka aruhusu kutoka kibali ili fedha hizo zikatumike kwenye ziara.**

WIKI iliyopita kuliibuka mjadala mzito kwenye mitandao ya kijamii baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, kuzuia kuidhinishwa Sh. milioni 47 zilizokuwa zitumike kwenye ziara ya Baraza la Madiwani na zaidi ya watumishi 60 akisema ni matumizi mabaya ya fedha.

Mtaka aliisoma barua ya maombi ya madiwani Oktoba 20, mwaka huu, iliyokuwa na kichwa cha habari; "Maombi ya kibali cha kufanya ziara ya mafunzo kwa waheshimiwa madiwani na watumishi wa halmashauri za jiji la Dodoma katika majiji ya Mbeya na Arusha.

Kwa mujibu wa barua hiyo, madiwani hao walitaka kujifunza elimu ya ukusanyaji mapato, usafi wa mazingira, uanzishwaji na uendeshaji wa shule za michepuo ya Kiingereza, uwekezaji wa mfuko wa elimu, utawala bora, usimamizi wa miradi ya maendeleo na utatuzi wa migogoro na changamoto zake.

"Kwa nini tutumie Sh. milioni 47 kwenda kujifunza namna ya kuendesha shule za English Medium? Serious? Na ukusanyaji wa mapato eti na kutunza mazingira, Rais atatufukuza kazi sisi wote na ataniuliza niko 'serious' kweli?" alihoji RC Mtaka.

Wakati RC Dodoma akizuia matumizi ya mamilioni ya fedha, tukashuhudia madiwani na watumishi wa jiji la Mbeya wakiruhusiwa kwenda kufanya ziara ya mafunzo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. Pia madiwani na watendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa nao tumesoma kwenye vyombo vya habari wamekwenda kwenye ziara ya mafunzo mkoani Morogoro.

Ziara zote hizo, yaani za madiwani na watendaji wa halmashauri za Mbeya na Iringa bila shaka zimetumia mamilioni ya fedha ingawa kiwango kamili kilichotumika kimebaki kuwa siri ya wakuu wa mikoa husika.

Baada ya RC Dodoma kuzuia fedha hizo kwenda kwenye mafunzo, mjadala mkali uliibuka kwenye mitandao ya kijamii baadhi wakifagilia hatua hiyo na wengine wakipinga wakitaka aruhusu kutoka kibali ili fedha hizo zikatumike kwenye ziara.

Niko upande wa wananchi ambao wanamuunga mkono RC Mtaka kwa uamuzi wake huo ambao nasema wazi kuwa ungefaa sana kuigwa na wakuu wa mikoa wengine.

Wanaopinga uamuzi huo niweke wazi kuwa hawana hoja ya msingi. Mfano mdogo niulize madiwani kwenye kata zao kuna kero ngapi ambazo hazijatatuliwa kwa ukosefu wa fedha?

Hivi hizo Sh. milioni 47 mfano zikigawanywa hata kwa kata mbili si zinaweza kusaidia kujenga mradi hata kama ni mdogo ambao utabaki kuwa kumbukumbu kwa wananchi kuliko ambavyo zingeenda kutafunwa na waheshimiwa hao kwa kugawana posho?

Nakumbuka kipindi cha serikali ya awamu ya tano, mambo hayo yalitoweka kabisa lakini sasa naona yameanza kurudi kwa kazi ya 4G. Wananchi tupinge kwa nguvu zote matumizi mabaya haya ya fedha zetu.

Nampongeza RC Mtaka kwa uamuzi huo na sisi wananchi ambao ndio walipakodi tuko nyuma yake japo najua wanasiasa hao watampiga madongo.

Alichokifanya RC Mtaka kinafaa kuingwa na wengine ambao ni wazalendo kwani haiwezekani na haikubaliki hata kidogo Sh. milioni 47 ziteketezwe kwa ajili ya kwenda kwenye ziara ya mafunzo.

Natambua kuwa mafunzo yana faida lakini kuna haja gani kwa madiwani wote wa jiji la Dodoma kwenda katika mafunzo hayo? Kwa nini wasiende wachache halafu wakirejea wasaidie kutoa elimu kwa wengine na fedha ambazo zingetumika zingekuwa kidogo.

Nilimsoma mkurugenzi mmoja mstaafu kwenye mitandao akisema bajeti ya mafunzo huwa inatengwa kila mwaka. Sikatai lakini ifike wakati tubadilike hali ya uchumi wa nchi haijakaa sawa kwa hiyo hata hizi kodi zinazotolewa na wananchi zitumike vizuri kwa ajili ya maendeleo na si kulipana posho tu.

Mwananchi anayelipa kodi anapoona madiwani wamekwenda ziara ya mafunzo na kulipana posho Sh. milioni 47 hivi atakuwa na nguvu na ari kulipa kodi huku akijua zinakwenda kutafunwa kwa waheshimiwa kulipana posho?

Kwa mantiki hiyo hata wakuu wa mikoa ya Mbeya na Iringa mtueleze madiwani na watendaji wa halmashauri katika mikoa yenu wametumia mamilioni mangapi kwenye ziara za mafunzo na je, zitaleta matokeo chanya au walienda kutumbua tu kama sio kula raha?

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**
**mwanakatwe 2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# ATHARI ZA MIGOGORO NA KUVUNJIKA KWA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Watoto katika makuzi yao hawajawahi kuona matendo mema ya baba na mama yao. Matokeo yake watoto hawa wakiwa watu wazima na wao wanafanya vivyo hivyo, kwani ndicho walichokiona na kujifunza kutoka kwa baba na mama yao. Wanakuwa ni watu waliotengenezwa kuwa hivyo walivyo.**

NDOA ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu na kitovu cha familia, jamii, taifa na malezi. Mungu alianzisha taasisi ya NDOA ili watu waingie, waipende na kuifurahia.

Hata hivyo, mambo yamekuwa kinyume kwa baadhi ya wanandoa. Siku hizi tunashuhudia migogoro mingi ya ndoa na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Kwa baadhi ya familia, ndoa imegeuka kuwa jela ya nyumbani na kusababisha upotoshwaji mkubwa juu ya kusudi na maana halisi ya ndoa na familia.

Hali hii imetokana na sababu zifuatazo:-

- Watu wengi wamevamia na kuingia katika ndoa wakiwa hawana ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa. Matokeo yake mwanandoa anakuwa kivuruge badala ya kuwa mlezi wa ndoa yake. Mbaya zaidi, wazazi wengi, ndugu na jamaa wameelekeza nguvu nyingi kwenye kuandaa sherehe kubwa za harusi, pasipo kuwaandaa vijana wao wa kike na kiume kuwa waume na wake bora. Hii imesababisha kuwa na wanandoa wenye msingi dhaifu wa ndoa kuanzia ngazi ya familia.

- Makuzi na malezi mabaya katika ngazi ya familia (negative parenthood experience). Wanandoa wengine walimeharibika kutokana na uzoefu mbaya waliopata kutoka kwa wazazi wao wakati wa utoto (negative parenthood experience). Wazazi wengi wamepoteza sifa ya kuwa kielelezo kizuri (role models) kwa watoto wao.

Watoto katika makuzi yao hawajawahi kuona matendo mema ya baba na mama yao. Matokeo yake watoto hawa wakiwa watu wazima na wao wanafanya vivyo hivyo, kwani ndicho walichokiona na kujifunza kutoka kwa baba na mama yao. Wanakuwa ni watu waliotengenezwa kuwa hivyo walivyo.

- Ulimbukeni na kukosa kufanya uamuzi makini wakati wa uchumba kuhusu nani wa kuoa na kuolewa naye. Vijana lazima wafahau kuwa, si kila mtu ana sifa ya kuwa mume au mke wa mtu. Wako walioruhusu watu wasiofaa katika maisha yao na wenye matatizo ya afya ya akili, ambao wameondoa furaha na kuua ndoto za maisha yao.

- Watu kumweka Mungu pembeni katika masuala yanayohusu uhusiano na ndoa. Hakuna usalama katika ndoa Mungu asipohusika. Matokeo yake ni maumivu katika uhusiano na ndoa zisizodumu.

Migogoro ya ndoa huondoa hisia za mapenzi na mvuto. Hali hii huchangia uwapo wa vitendo vya ukatili ndani ya ndoa na vifo. Vyombo vya habari vimekuwa vikisika na kutoa habari za vitendo vya mauaji ndani ya ndoa katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Migogoro na kuvunjika kwa ndoa huathiri afya na ustawi wa familia.

Athari hizi haziwahusu wanandoa tu, bali wazazi ambako wanandoa hao wanatoka pia. Athari za migogoro na kuvunjika kwa ndoa ni kubwa zaidi kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo kwani huathiri makuzi yao na kusababisha mmomonyoko wa maadili. Migogoro na kuvunjika kwa ndoa huleta msongo wa mawazo wenye athari mbaya (stress- leading to negative effects).

Pia athari zake ni kubwa kiroho, kiuchumi, kisaikolojia na kiafya. Zaidi sana, huathiri ufanisi wa utendaji kazi na husababisha ongezeko la watoto wa mitaani, ajira na mimba za utotoni.

Kuwa baba na mama ni jukumu la heshima. Kila mzazi afahamu kuwa, katika kutekeleza jukumu la malezi kwa watoto wake anawajibika kwa Mungu aliyempatia zawadi ya watoto alionao. Kwa hiyo wazazi wasiwakoseshe watoto wao. Wazazi wanaojitambua huruhusu watoto wao kujifunza mambo mema kutoka kwao.

Malezi yao bora huwakuza watoto katika hali salama, ambayo itawawezesha kujisimamia katika maisha yao na kufanyika baraka kwao wenyewe, familia na jamii kwa ujumla. Watoto waliolelewa vibaya hawako salama sana, kwani ni rahisi kusombwa na chochote kitakachopita mbele yao kwa kuwa dhamiri zao zinakuwa butu kukabiliana na changamoto na mazingira tofauti. Mtoto mwenye malezi mabaya ni mzigo wa baba na mama yake.

Wanandoa wajifunze namna ya kusimama katika nafasi zao ipasavyo na kujiepusha kutengeneza mazingira ya migogoro isiyo ya lazima. Waepuke kufanya uamuzi ya haraka ya kutaka kutengana au kuachana.

Mtu anapoamua kumwacha mwenzi wake kwa sababu ya kasoro zake, ajiulize anachotafuta ni nini? Katika maisha mtu aliyekamilika na asiyekosea hayupo. Wanandoa wanashauriwa kutafakari kwa makini na uangalifu mkubwa matokeo ya uamuzi wao ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza katika maisha yao na makuzi ya watoto wao.

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

OKTOBA 31, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana


Jumapili






Ukurasa 14

**Tumia njia rahisi kuimarisha nyusi zako**




KATUNIKA

Ukurasa 16










# Ukialikwa harusini, alikika kistaarabu

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | A | S | H | A |
| ■ | E | ■ | ■ | U | ■ |
| U | P | E | ■ | R | ■ |
| ■ | O | ■ | P | U | A |
| ■ | N | ■ | ■ | M | ■ |
| S | I | M | B | A | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
JAA, DAU, SHIDA, BANGI, DAWATI, SHAMBA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

**Alichokifanya daktari**

MTOTO Juma alikwenda mtoni na mama yake kuchota maji , walipokuwa wakiendelea kuchota maji juma aliona kiota cha ndege kikielea majini. Katika kudadisi aliamua kumuuliza mama yake.

Juma: Mama ona kile kinachoelea majini

Mama: Ni kiota cha ndege kile nadhani kimeanguka majini.

Juma: Mama yani hataka kiota kimeundwa kwani mwalimu ametufundisha kila kieleacho majini kimeundwa.

Mama: Hapana mwanangu kuna takataka na majani yanaelea pia, huo ni masemo unaoelezea kila kilicho bora kuna jitihada imetumika.

Swali

Mnyama gani mwenye damu baridi anayeishi mtoni.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mbinu za kisaikolojia kutatua migogoro yako kimaisha

KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya mwisho ya mada yetu kuhusu vyanzo vya migogoro na jinsi ya kuitatua. Wiki iliyopita niligusia uzembe na hofu ambayo nitaiendeleza leo na kushauri nini cha kufanya.

Hofu ni moja ya vyanzo vya migogoro katika maisha yetu na ndio maana watu wengi wanashindwa kufanya uamuzi. Mahakamani, kwa mfano, watu wengine wanashindwa kufanya uamuzi wakiogopa pengine vitisho kwamba ukifanya hivi, kitakupata kitu fulani.

Anaweza kukutishia mtu eti kwamba huwezi kuamka kesho. Huo ni mgogoro uliotengenezwa ambao hukuacha unawaza, sasa itakuwaje. Endapo utaacha kuogopa utaanza kujisikia amani na kuishi uhalisia wako.

Kwa hiyo, ni vizuri endapo utaweza kuikataa hofu kwa kuwa siyo sehemu yako. Wewe haujaumbwa na hofu ila unaitengeneza mwenyewe. Wapo watu wana hofu ya umri unaongezeka na mambo hayajakaa sawa.

Usijilinganishe na watu wengine. Jitofautishe na hakikisha kila siku unaongeza thamani kwenye maisha yako. Ongeza thamani kwa kile unachokifanya ili matokeo yaweze kuwa dhahiri.

Wako pia watu wana hofu pale anaposema, kila ninapokaa nakuwa mtu muoga na mwenye wasiwasi. Sikia nikuambie msomaji wangu; Hivi kuna faida gani ya kuwekeza nguvu au akili yako katika vitu ambavyo havipo?

Watu wengi wanateseka kwa vitu vya kufikirika, havipo unaogopa? Unatengeneza maswali, unajipa majibu? Nani kakuambia hivyo? Ni kwamba wewe umetengeneza hayo na si matokeo halisi ya kile ambacho pengine ungekifanya kingekuwa tofauti.

Labda ni mgogoro binafsi unajitengenezea kwamba kazi hakuna. Nani kakuambia kazi hakuna. Je, umetafuta? Wakati mwingine inashangaza kwa sababu unakubali kuishi mawazo ya watu wengine badala ya kuishi maisha yako! Hicho pia ni chanzo cha migogoro inayoweza kukutesa, ukashindwa kuwa bora zaidi. Msomaji, hadi sasa tumekuwa tukijadili suala zima la migogoro kisaikolojia. Kipengele ni athari za migogoro ambazo zinatokea. Tumeshaona chanzo na pia misingi ya migogoro.

Chanzo kingine cha migogoro katika maisha yetu ya kila siku ni udumavu. Unapoweka vitu vingi mabegani mwako hutaweza kukimbia. Hutaweza kukimbia kwa kasi, utashindwa kuendelea. Kwa hiyo migogoro inapotokea unaweza kudumaa kifikra na pia kimwili kwa vile umeshindwa kuwa mtu wa tofauti.

Pia migogoro inaweza kusababisha vifo. Wapo watu hutengeneza visasi. Ni hatari zaidi kwa sababu endapo utashindwa kutatua migogoro husika unaweza kumdhuru mtu mwingine kutokana na kuwa na hasira muda wote na kuwa na ile hali ya kutaka kusuluhishwa lakini hupati mtu sahihi kukusaidia.

Migogoro pia hupelekea vita na fujo endapo watashindwa kuelewana hivyo kuishia kupigana. Wasipokubaliana, fujo yaweza kutokea na kuleta madhara kwa wahusika au kusababisha uharibifu wa mali za gharama kubwa.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa kisaikolojia, Charles Kalungu, kuna njia kama mbili za kisaikolojia ambazo zinaweza kutatua migogoro yako. Njia ya kwanza ni kupitia upatanishi.

Mpatanishi ni yule mtu anayeweza kuwakutanisha watu wawili kutoka sehemu tofauti ambao wanahitilafiana na kuweza kuwaunganisha pamoja. Pengine walikuwa kwenye uhusiano unawaleta pamoja na kuwasikia kila mmoja nini alichokihitaji zaidi au ni nini alikuwa hapati na mwisho unaweza kuwapatanisha.

Wengine huwa wanakataa kwa sababu ya hasira. Hivyo ni vema ukamtafuta mtaalamu wa afya ya akili kuweza kurejesha tena hali ya amani katika mgogoro husika.

Njia nyingine ni kusuluhisha akiwamo msimamizi. Kwa mfano wapo watu wenye kesi Mahakama ya Kazi kusuluhishwa au kupatanishwa. Pale unaweza kushinda au kushindwa lakini mwishoni mmesuluhishwa.

Kama utapata msuluhishi sahihi, anaweza kukusaidia kusuluhisha mgogoro wako na maisha yakaendelea. Huwezi kuendelea kama una migogoro na watu. Kama una madeni lipa, siyo unakaa na kujisahaulisha. Samehe watu wengine, tafuta amani na wengine ili upige hatua kubwa.

Unapokuwa na migogoro unapiga hatua moja unarudishwa tena. Tatua migogoro mapema uweze kufika mbali. Vinginevyo yaweza kuwa vigumu sana kupiga hatua. Raha ya maisha ni kufurahi na huwezi kufurahia maisha ukiwa na shaka.

**Niishie hapa msomaji wangu tukutane tena wiki ijayo. Una maoni, kisa cha kimaisha? Tuma ujume mfupi 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Vikwazo wawekezaji nishati jadidifu viangaliwe

NISHATI jadidifu ni rafiki kwa mazingira kwa kuwa haizalishi hewa ukaa ambayo husababisha kuharibika kwa tabaka la dunia kiasi cha kusababisha mabadiliko yanayoonekana sasa duniani ikiwamo kubadilika kwa vipindi vya mvua, mafuriko, ukame wa muda mrefu na majanga mengine.

Kwa sasa mataifa yanayochangia hewa ukaa duniani ni China ikifuatiwa na Marekani. Mataifa haya yanazalisha na kutumia nishati kwa ajili ya usafiri, viwanda na matumizi mengine kwa kiasi kikubwa.

Aidha, kwa sasa dunia inazungumzia umuhimu wa kuwa na nishati jadidifu isiyoharibu mazingira ambayo ni umeme unaozalishwa kwa upepo, sola, joto ardhi na maji vyanzo ambavyo Tanzania inavyo na baadhi vimeendelezwa.

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felschemi Mramba, anasema serikali imejiwekea malengo ya kuzalisha megahat 550 za nishati jadidifu ifikapo 2023 ikiwa ni sekta binafsi kuzalisha megawati 400 na Shirika la Ugavi wa Umeme nchini (TANESCO) megawati 150.

Aidha, anasema hadi kufikia 2025 wataongeza megawati zingine 600 kutoka vyanzo vya jua, upepo na maporomoko madogo ya maji huku joto ardhi pekee likitarajiwa kuzalisha megawati 200.

Anasema ili kufikia malengo haya wanahamasisha wawekezaji kuwekeza eneo hilo, ili kuendana na matakwa ya dunia ya kuachana na nishati zinazochafua mazingira kama petroli, dizeli na makaa ya mawe na kuelekea kwenye nishati jadidifu.

Kwa mujibu wa Mramba, uzalishaji wa umeme nchini kwa sasa ni megawati 900 za umeme utokanao na gesi, megawati 508 za maji na 58 za vyanzo vya nishati jadidifu, ndiyo maana nguvu kubwa inaelekezwa huko ili kuongeza kiwango cha umeme unaoingia kwenye gridi ya taifa.

Anasema mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ukikamilika utazalisha megawati 2,115 na kuifanya nchi kufikia umeme wa megawati 4,000 na iwapo nishati jadidifu itaimarishwa zitafikiwa megawati 5,000 ifikapo 2025.

Aidha, anathibitisha kuwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCOO haliwezi kuhudumia wateja wote kwa kuwa wakati mwingine kuna maeneo kupeleka umeme ni gharama kubwa ndiyo maana wanapatikana wawekezaji wanaowekeza huko na kuzalisha umeme ambao huuzwa kwa wananchi moja kwa moja.

Hadi sasa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati ya mimea yaani mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia na shughuli nyingine ambao huchangia uchafuzi wa mazingira.

Pia asilimia nane hadi 10 ya matumizi ya nishati ya umeme ni madogo kulinganisha na mahitaji na ndiyo maana msukumo mkubwa umekuwa kwenye nishati jadidifu ambao utaisaidia nchi kwenye hifadhi ya mazingira.

Kilio cha waliowekeza kwenye sekta hiyo akiwamo mwekezaji wa kampuni ya Rift Valley ni utitiri wa vibali ili mtu afanikiwe kuwekeza kuwa si chini ya 30 na vinapatikana maeneo tofauti, hali inayowaongezea gharama na usumbufu.

Mwekezajii huyo ni wa kwanza kuwekeza kwenye umeme wa upepo na pia anazalisha umeme kwa kutumia maji ambao huingiza kwenye gridi ya taifa na mwingine unasambazwa kwenye vijiji 20 ambavyo havijawahi kupata umeme tangu kuanzishwa kwake.

Ni muhimu mamlaka husika zikasikia kilio cha wawekeza hawa kwa kuwa wana nia lakini usumbufu wanaokutana nao ni mkubwa huku baadhi wakinyimwa kuzalisha umeme wao kwa kuwa tayari kuna umeme wa TANESCO.

Katika wakati huu ambao Rais Samia Suluhu Hassan, atahutubia mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa utakaojadili athari za mabadiliko ya tabianchi (COP 26), ni muhimu serikali ikaangalia uwezekano wa kurahisisha mazingira hasa kwa mwekezaji kupata huduma zote kwenye eneo moja.

Kidogo kidogo Tanzania itaingia kwenye rekodi ya nchi zilizofanikiwa kuachana na nishati inayozalishwa kwa mafuta au makaa ya mawe lakini kuacha kutumia mkaa kama nishati ya kupikia ambao kunachangia uharibifu mkubwa wa mazingira.

Tanzania imebarikiwa maeneo yanayofaa kuzalisha umeme wa upepo, jua na joto ardhi lakini bado uwekezaji kwenye sekta hiyo ni mdogo, lakini ikiwa nguvu itaelekezwa huko tutafika wakati matumizi ya mafuta yatakuwa madogo.

Hadi sasa utafiti umeonyesha maeneo yanayofaa kuzalisha umeme wa jua na upepo ni Mbeya, Songwe, Singida, Shinyanga na Dodoma na kwamba wapo wawekezaji waliojitokeza kuonyesha nia ya kuwekeza huko.

Hadi sasa si maeneo yote yanategemea umeme wa maji kutoka TANESCO bali unaozalishwa kwa mafuta kama Kigoma, Rukwa, Katavi na Mafia huku baadhi ya visiwa mkoani Mwanza vikitegemea nishati jadidifu.

Ni matarajio ya Watanzania kuwa ushiriki wa Rais COP 26 utaifungulia Tanzania fursa za uwekezaji, kujulikana kimataifa hasa kwa jitihada za kuzalisha nishati jadidifu kama ilivyo kwa Kenya na Afrika Kusini ambazo zinazalisha nishati hiyo kwa kiasi kikubwa.

HARUSI











Mei 22, mwaka huu, ilikuwa siku ya furaha kwa Bwana Octavian Kiwale na Beatrice Mushi, baada ya kufunga ndoa katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Peter Clavery, Mbezi Luis na kufuatiwa na tafrija iliyofanyika ukumbi wa Kiramuu, Mbezi Beach, Dar es Salaam.

# MITINDO

Na Mary Geofrey









## Ukialikwa harusini, alikika kistaarabu

UKIALIKWA alikika, hii ni kauli ambayo imetawala katika miaka ya hivi karibuni hasa kwa wageni waalikwa wa shughuli kama harusi, sendoff na kitchen party.

Imekuwa kawaida kwa mtu anayependa kupendeza na kwenda na wakati inapotokea kuwa na shughuli ya mtu wake wa karibu au anayemfahamu kujipanga kuwa atoke vipi.

Suala la mchango ni la kwanza lakini kuhudhuria ni zaidi ya mchango kwa sababu watu huingia gharama kubwa zaidi ya alichochangia ili kuhakikisha siku hiyo anatokelezea.

Miaka ya nyuma ilizoeleka wanaopania na kutaka kutokelezea kwenye shughuli za watu wakiwa wapya kimavazi na mitindo ni wanawake ila siku za karibuni hata wanaume nao wamo.

Nini ufanye mwalikwa

Kabla ya kuamua uvae nini mwaalikwa unatakiwa utambue kuwa kuna rangi za mwaka ambazo ndizo zinakuongoza utoke vipi.

Pia unatakiwa uchague aina ya mitindo kulingana na wakati tuliopo, uangalie vazi ambalo utakuwa huru kucheza na kusherehekea vyema shughuli unayohudhuria.

Usipanie sana ukajikuta unashona au kununua nguo ambayo hautakuwa huru na kuishia kukaa kwenye kiti bila kunyanyuka mwanzo mwisho.

Kuna staili ya watu kushona mkia, ni vizuri mkia ukawa wa saizi, usizidishe kiasi ukaanza kuonekana msumbufu ukumbini.

Shona saizi ambayo utaweza kukaa, kucheza na kutembea bila kuomba msaada wa jirani akushikie nguo yako au awe na kazi ya kukunasua unapokwama.

Hakikisha pia kama unaenda harusini utambue rangi nyeupe ni ya bibi harusi, usishone nguo nyeupe ukaanza kuonekana wewe ndio unaolewa na wakati unajua wazi shughuli si yako. Kama utavaa nyeupe hakikisha haiendani na nguo au mitindo ya maharusi.

Zingatia pia viatu ambavyo ukivaa unaweza kutembea mwenyewe bila kutegemea msaada wa viti na meza.

Ukialikwa alikika kistaarabu kwa kuvaa nguo ambayo haiwakaraishi wengine na utatokelezea vizuri tu.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Tumia njia rahisi kuimarisha nyusi zako



IMEKUWA tabia ya wanawake wengi kuweka kope za bandia bila kujali madhara yanayoweza kuwapata kutokana na matumizi hayo.

Leo tunawaletea njia rahisi ya kukuza nyusi au kope zako kwa njia ya asili ukiwa nyumbani kwako.

Huna haja ya kwenda saluni kuweka kope kwa gharama kubwa na kuhatarisha usalama wako.

Vitu vinavyotumika unaweza kuvinunua ukawa navyo nyumbani kwako hasa brashi la kupakia maskara.

Faida ya kutumia njia hii kukuza nyusi au kope zako ni kwamba zinakua zako moja kwa moja kwa hiyo mwonekano huu ni wa milele.

**Hatua za kufanya**

Safisha vizuri brashi yako ya maskara ili kuondoa ule weusi.

Ukishasafisha hakikisha unaikausha kwa kitambaa au taulo safi kabla ya kuanza kutumia.

Kama ulikua umepaka make-up au umepaka mafuta yoyote nawa ili uso wako uwe mkavu.

Chukua brashi yako na uiweke mafuta ya Vaseline na uanze kupaka kwenye nyusi zako au kope.

Fanya hivi kwa muda wa wiki na utaona matokeo unaweza kuendelea kufanya mpaka pale utakapo ridhishwa na urefu wa nyusi au kope zako.

Hakikisha unapaka mafuta hayo kwenye kope zako wakati wa usiku.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Maajabu ya tango, tumia kama mlo au juice



TANGO ni tunda lenye maji kwa asilimia 95 na lililo rahisi katika kulitengeneza.

Tango pia lina ngozi nyembamba ambayo ni rahisi katika kutengeneza juisi yake.

Ili kutengeneza juisi ya tango, chukua tango moja au zaidi, lioshe vizuri kisha katakata vipande tayari kwa kusaga kwa mashine au kwa kutwanga kwenye kinu maalum.

Changanya na maji safi kiasi ili kupata juisi kiasi cha glasi moja.

Unaweza kuweka sukari kiasi kidogo sana ambayo haizidi kijiko kimoja kwa glasi ili kupata ladha au weka asali kijiko kidogo kimoja.

Utapata matokeo mazuri na ya haraka kama ukinywa juisi yako kila siku asubuhi kabla ya kula kitu chochote.

Vile vile, unaweza kujiwekea mazoea ya kula tango kwa njia mbalimbali kama vile kuchanganya na saladi, kachumbari au kutafuna lenyewe mara kwa mara, kwa sababu faida zake ni nyingi.

**Faida zake**

Tango lina kirutubisho cha potasiamu ambacho husaidia kupunguza mafuta mabaya mwilini (cholesterol), huimarisha misuli ya mwili na bila kusahau husaidia usagaji wa chakula tumboni, hivyo kuondoa tatizo la ukosefu wa choo.

Virutubisho vilivyomo kwenye tango pia hutoa afueni kwa mtu mwenye matatizo ya ini, kongosho, figo na matatizo katika kibofu cha mkojo.

Tango pia lina kiwango kingi cha vitamin C, hivyo kuwa na uwezo mkubwa wa kuondoa matatizo yatokanayo na ukosefu wa vitamin C kama vile kutokwa na damu kwenye fizi, upungufu wa damu kwa watoto wachanga na kuota meno na mifupa vibaya.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba

KILA uchao tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna mbalimbali yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya sasa.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yanayofanyika leo na yale tatakayofanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa.

Leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Sakafu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba hasa pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo msanifu majengo, David Kashozi, anayaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.

Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake na jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana zingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasema.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.



## Namna ya kugeuza mboga kuwa maua



JE, unafahamu kwamba unaweza kutengeneza bustani ya mboga nyumbani na kuipendezesha nyumba yako? Basi kwa kufuata dondoo zifuatazo unaweza kupanda mboga nje ya nyumba na kuwa kama maua.


1: Panda mchicha katika mitungi inayozunguka nyumba au njia ya kuingia ndani. Panda aina tofauti ya mchicha ili kutoa rangi za majani zinazovutia.

2: Panda mboga ya maboga kwenye matairi ya gari, unaweza kuweka chini au kuning'iniza juu ili kuweka mandhari ya kupendeza.

3: Kwa wale wenye eneo kubwa unaweza kuweka matuta pembeni ya njia ya kuingia ndani na kisha ukapanda mboga tofauti kama matembele, mgagani au spinachi.

4: Kama unapendelea mboga zisizotambaa basi unaweza kupanda pilipili au mnavu kwa kutumia mifuko pembeni ya nyumba au barazani.

## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
HE!
VIOO-NGOZ
WABABAIFU
NITAPATA WAPI USHAURI MZURI NIMEKOPA DENI LINANISHINDA
MUWAHI BWANA JELA
KAMA NDIO KUPATA JANAUME 'BOMU' SISI NI VINARA!
JANAUME GANI KILA SIKU KAZI YA KULIOKOTA BAR KAMA KISODA CHA BIA!
HAKUNA NAULI YA 'BUKU' ZAIDI YA MIA INE!...
KAMA ULIJUA HII NI PRAIVETI UNGEPITA NA ZAKO.
UNAJUA HUYU JAMAA ANAJISHAUA, KWANI USINGESIMAMA NA KUTANGAZA UENDEKO NANI ANGEPANDA?
TUPELEKE USIJE UKAYAZUA MENGINE!
SICHUKUI NAULI ZENU.
MUNGU AKUBARIKI TWENDE
UKIWAENDEKEZA HAWA UNAWEZA KUSOMEWA 'HITIMA' UKAZANIWA UMEFARIKI KUMBE UPO "KIZUIZINI!"
NYUMBA NDOGO
EMBU NAMBIE ILE BIA ULIONINYWEA KISHA UKAYEYUKA, MUAFAKA WAKE UKOJE?
MH!!!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIONA KAPENDEZA, MWENZAKO KAWEKEZA

# HABARI KIMATAIFA




Viongozi wa nchi zilizostawi kwa viwanda na zinazoinukia kiuchumi - G20 wamewasili mjini Roma Italia, kuhudhuria mkutano wao wa kilele, ambao ni wa kwanza kukutana tangu mlipuko wa virusi vya corona.**DW**

## Modi amwalika Papa Francis India

**NEW DELHI,** INDIA

WAZIRI Mkuu wa India, Narendra Modi amemualika kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis kuizuru India.

Mwaliko huo aliutoa jana baada ya kukutana na Papa Francis kwa mara ya kwanza, pembezoni mwa mkutano wa kilele wa viongozi wa kundi la nchi zilizostawi na zinazoinukia kiuchumi za G20, mjini Rome.

Modi alisema amepata fursa ya kuzungumza mambo mengi na Papa alipomtembelea kwenye makaazi yake mjini Vatican.

Mara ya mwisho kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani kuizuru India ilikuwa mwaka 1999. India nchi yenye waumini wengi wa Kihindu, ina takriban Wakristo milioni 28.

Kabla ya mkutano wa viongozi hao wawili, redio ya Kanisa Katoliki iliripoti kuwa maombi ya awali yaliyotolewa na Vatican kutaka Papa aizuru India, yalikataliwa na nchi hiyo.

Papa Francis alitarajiwa kutoa wito kwa Modi kuongeza juhudi za kukabiliana na hali ya kutovumiliana kidini.

**DW**

## Blinken: Ghasia dhidi ya maandamano ya amani nchini Sudan hazikubaliki

**WASHINGTON D.C,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, amesema vikosi vya usalama vya Sudan vinapaswa kuheshimu haki za binadamu na kwamba ghasia dhidi ya maandamano ya amani hazikubaliki.

Kauli hiyo aliitoa jana katika ukurasa wake wa Twitter na kusema kuwa, Marekani inaendelea kusimama na watu wa Sudan katika mapambano yao yasiyo ya vurugu kwa ajili ya kutetea demokrasia.

Upande wa watu wanaopinga mapinduzi ya kijeshi nchini Sudan walitisha maandamano ya nchi nzima jana wakitaka kurejeshwa kwa serikali ya kiraia kwa lengo la kuirudisha nchi hiyo kwenye njia ya kidemokrasia baada ya miongo kadhaa ya utawala wa kiimla.

**DW**

# Uingereza kutoa mamilioni chanjo COVID-19 kwa nchi masikini

**LONDON,** UINGEREZA

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amesema nchi yake itachangia dozi milioni 20 za chanjo ya virusi vya corona aina ya AstraZeneca kwa nchi zinazoendelea, kama sehemu ya juhudi za kugawana chanjo na nchi ambazo hazijapata chanjo hiyo.

Ahadi hiyo aliitoa baada ya kuwasili mjini Rome kuhudhuria mkutano wa kilele wa viongozi wa kundi la nchi zilizostawi na zinazoinukia kiuchumi za G20 ambao unaanza jana.

Uingereza ilisema dozi milioni 10 zimepelekwa kwenye mpango wa kimataifa wa COVAX, wa kununua na kusambaza chanjo za bure kwa nchi maskini zaidi duniani, na milioni 10 zaidi zitatolewa katika wiki zijazo.

Johnson alizitaka nchi zenye uchumi mkubwa za G20 kuhakikisha ulimwengu wote umepata chanjo ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022.

Alisema kipaumbele chao cha kwanza kama G20 kinapaswa kuendelea na usambazaji haraka wa chanjo ulio sawa na wa kimataifa.

**DW**

# Vikosi vya Tigray vyaudhibiti mji muhimu jimbo la Amhara

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

VIKOSI vya waasi katika jimbo la Tigray nchini Ethiopia vimesema vimeudhibiti mji muhimu wa Dessie ulioko kwenye jimbo la Amhara. Katika jimbo hilo, maelfu ya watu wa jamii ya Amhara wamekuwa wakitafuta hifadhi kutokana na kuongezeka kwa mapigano. Msemaji wa chama cha Ukombozi wa Watu wa Tigray, TPLF, Getachew Reda, aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba wapiganaji wali-ivifurumusha vikosi vya serikali kutoka kwenye mji huo na walikuwa wanaelekea kwenye mji wa Kombolcha.

Getachew aliongeza kusema kuwa vikosi vya Tigray viliwakamata wanajeshi kadhaa wa Ethiopia.

Msemaji wa serikali ya Ethiopia, Legesse Tulu hakupatikana mara moja kuzungumzia suala hilo.

Hata hivyo, Reuters haikuweza kuthibitisha kuhusu madai hayo ya TPLF.

**DW**

# Mfungwa adungwa sindano ya kifo Marekani

**WASHINGTON D.C,** MAREKANI

JIMBO la Marekani la Oklahoma limetekeleza adhabu ya kifo kwa kumdunga sindano ya sumu iliyomuua mfungwa mara ya kwanza baada ya miaka sita tangu adhabu hiyo ilipotekelezwa.

Walioshuhudia tukio hilo wanasema John Grant - mwanaume (60), alionekana akitetemeka na kutapika baada ya kudungwa sindano hiyo. Hukumu hiyo ya kifo ni ya kwanza Oklahoma tangu mipango ifanyike mipango ya jimbo hilo kusitisha adhabu ya kifo.

Mawakili wa Grant wanadai kuwa matumizi ya sindano za midzolam ni adhabu isiyo ya kawaida, inayokiuka haki zake za kikatiba

**BBC**

SAFU

MAKALA

# SI KILA USHAURI UNA MANUFAA KWAKO



Na Magabilo Masambu

**Ukiwa na uwezo mdogo wa fikra dhidi ya aliyekushauri juu ya jambo fulani, basi kuna hatari ya ama kukataa ushauri mzuri au kukubali ushauri mbaya.**

NI kweli kwamba kila mtu ameumbwa na vipawa mbalimbali, hivyo anaweza kuwa anafahamu mambo mengi kutokana na uwezo huo. Pamoja na vipawa hivyo, hawezi kuwa anaelewa kila kitu.

Hilo liko wazi kwa sababu atakuwa na uwezo wa kuelewa katika maeneo pekee aliyobarikiwa nayo.

Tofauti ya binadamu na wanyama wengine kama mbuzi, kondoo na punda, ni kitu kinaitwa utashi. Utashi ni uwezo wa kutambua baya na jema, yaani baya na jema likifanyika uwe na uwezo wa kutambua na kuchukua hatua katika njia sahihi kulipokea ama kulikataa.

Nakubali kwamba wako watu wanaoyaona mambo kwa usahihi kabla ya kutokea na kuona wanalo jukumu la kutoa ushauri yasifanyike au yafanyike kwa namna ambayo wanafikiri yatazuia mambo fulani mabaya yasitokee. Upande wa pili, wako wanaoyaona mambo mazuri yakiwa mbele lakini kwa makusudi wanachukua hatua ya kutoa ushauri ili yale mazuri yasitokee.

Unaweza kupewa ushauri wa kisiasa, kielimu au kijamii. Ushauri kwa asili yake huwa hauzingatii taaluma ya mtu. Unaweza kupewa ushauri na mtu yeyote na kazi itakayokuwa mbele yako ni moja tu, kuupokea au kuukataa. Kitendo cha kuchagua kama umeupokea au umeukataa kinategemea uwezo wako wa fikra na utashi wako katika yale uliyoshauriwa.

Ukiwa na uwezo mdogo wa fikra dhidi ya aliyekushauri juu ya jambo fulani, basi kuna hatari ya ama kukataa ushauri mzuri au kukubali ushauri mbaya. Ushauri wowote huwa hauitaji sana majadiliano, bali tafakuri ya ndani kabisa kabla hujachukua uamuzi wa kuukataa au kuukubali.

Kuna ndoa nyingi sana zimevunjika kwa sababu ya ushauri wa watu wa pembeni. Wengine wanatumia uzoefu wa matatizo yao kuwa matatizo yako, furaha zao kuwa zako, uhusiano wao kuwa wako. Jambo la msingi hapa ni kutambua kwamba kuna baadhi ya mambo ni ya kipekee hayafananishwi na mengine.

Katika eneo la siasa, ushauri umeleta matatizo makubwa sana duniani na hasa katika Afrika. Wako watu wameumizwa vibaya kwa sababu ya ushauri unaotokana na watu wengine. Kuna wengine wanafikiri nchi zao zilivyo ndivyo nchi zingine zilivyo pia. Mwenyezi Mungu alikuwa na makusudi ya kuifanya Amerika iwe tofauti na Uingereza au Tanzania kuwa tofauti na Rwanda.

Maana yake ni kwamba kinachofanyika Amerika kitakuwa tofauti na kinachofanyika Uingereza na kinachofanyika Tanzania lazima kiwe tofauti na kinachofanyika Uganda, hivyo yatakuwa makosa makubwa kuchukua uzoefu wa Zambia kuiendesha Malawi. Tafsiri yake ni kwamba Rais wa Zambia akipewa ushauri wa namna ya kuiendesha nchi yake kutoka Botswana lazima achuje kwa kutumia utashi wake juu ya jambo gani alitekeleze au aliache.

Eneo la elimu pia limeathirika zaidi na ushauri wa watu. Leo hii kuna wazazi wakimwona jirani ameanza kazi fulani baada ya mwaka mmoja kajenga nyumba na anamiliki gari, lazima wamshauri kijana wao akasome alichosomea jirani yao huyo, bila kufahamu kwamba inawezekana kipato chake hakitokani tu na ujira wake.

Wako watu ambao wamesoma kozi fulani na baadaye kugudua kwamba walikosea kuchagua. Ni kweli kwamba wako waliokosea kwa sababu walichagua kwa kutojua na kwa kutoshauriwa japo wengine walikosea kwa kushauriwa na watu wao wa karibu lakini baadaye wamekuja kubadili.

Nathibitisha hili kama ambavyo tumesikia juzijuzi kijana mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akitoa ushuhuda alivyoshindwa kozi ya kwanza na baadaye kujiunga na kozi nyingine chuoni hapo, iliyomfanya akawa kinara katika matokeo yake. Inawezekana kabisa alishauriwa kujiunga na kozi ya kwanza ya makenika ambayo hakuwa na uwezo nayo.

Tukubali ushauri wa watu lakini kabla ya kuutekeleza unahitajika umakini, tahadhari lakini tafakuri ya kutosha.Tukipokea kama ambavyo dodoki linanyonya maji kwenye bakuli, basi kama si leo ni kesho tutakuwa tunajutia uamuzi wa ushauri wenyewe.

Wakati mwingine tunatekeleza ushauri wa maadui wa wale wanaotushauri. Hatuna sababu ya kubeba maadui wa watu wengine kwa mwavuli wa ushauri kwa sababu Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema: "Mtu yeyote mwenye akili, akikushauri jambo la kipumbavu na anajua ni jambo la kipumbavu ukilikubali atakudharau."

Kuna wengine wanakushauri ili wapate cha kukusema nacho baadaye. Ubaya wa ushauri mambo yakiharibika washauri huwa hawajitokezi kusema sisi ndiyo tulimshauri badala yake hugeuka kuwa wanasihi uchwara, lakini yakiwa mazuri watajitokeza wengi na kwamba alifanyia kazi ushauri wetu.

Kwa hiyo jambo la muhimu kuwa makini na kila aina ya ushauri unaopewa kwa sababu si kila ushauri una manufaa kwako. Mwingine ni wa kukubomoa au kubomoa nyumba yako na mwisho majuto anakuwa ndiye mjukuu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Waliopotea kwenye mdundiko wasimulia*



Na Adam Fungamwango

BAADA ya wiki iliyopita kutoka kwa makala ya safu hii yenye kichwa cha habari 'Mdundiko ulivyopoteza watoto', wasomaji wengi walionekana kuvutiwa nayo huku baadhi wakiniandikia visa mbalimbali vilivyowahi kutokea huko nyuma lakini pia waliwahi kupotea huko nyuma nao wakaibuka na kusimulia.

Katika maeneo ya mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, kulikuwapo ngoma maarufu iliyokuwa inaitwa mdundiko. Umaarufu wake ulikuwa kwenye miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa 1990, baada ya kumalizika kipindi cha umaarufu wa ngoma ya 'gombe sugu'.

Nilisema kuwa wengi waliokuwa wanasombwa na ngoma hiyo ni wanawake na watoto na staili ya ngoma hii haikai sehemu moja. Ni ngoma inayotembea. Inaweza kutoka Ilala ikaenda hadi Msasani au Mbagala hadi Buguruni. Inakatiza barabara na mitaa yake.

Kila inapopita, kinamama wanatoka majumbani kwao ili kuangalia, kucheza au kuondoka nayo moja kwa moja wakicheza na kuburudika. Watoto nao ni hivyo hivyo.

Pamoja na sifa kubwa, nikazitaja athari zilizokuwa zikipatikana kutokana na ngoma hiyo. Nayo ni kupotea kwa watoto. Pia ni wanawake kuunguza mboga na wakati mwingine kuingia mzozo na waume wao, ikiwemo kupigwa.

Watoto waliikimbilia na kwenda kuangalia na kucheza. Tatizo wanapochoka na kujitoa kwenye kundi, wakajikuta wapo mbali na nyumbani na hawajui njia waliopitia hadi kufika hapo. Kifupi tu ni kwamba wanakuwa wamepotea. Hata wale wanaofika mwisho, pia wanakuwa hawawezi kurudi walikotoka. Wazazi wanapata shida ya kuwatafuta. Hadi kupatikana ni lazima kazi kubwa ifanyike, au vituo vya polisi vihusike. Wakati huo simu hakuna.

Kwa upande wa kinamama hao hawapotei. Tatizo ni kwamba wakati mwingine wanakuwa wamebandika mboga, nyama au maharagwe. Mdundiko unapita. Anakimbilia, anacheza au kufuatana nao kwa robo, nusu au kilometa moja. Akirudi nyumbani mboga imeungua. Wakati mwingine hata kama hajaacha mboga jikoni, akirudi anamkuta mumewe amesharejea kazini. Nyumbani hakukuta mtu. Mke hata akijitetea alifuata ngoma, bado itaonekana ni tatizo kwani wakati mwingine mama amefuata ngoma mlango ameacha wazi.

Jambo hili liliwasukuma wengi kuniandikia, wakiwamo waliowahi kupata mkasa kutokana na ngoma ya mdundiko.

Wako walioniambia kuwa kwa wakati ule kwa sababu simu hazikuwapo, basi watoto walikuwa wanaweza kupotea kuanzia wiki moja hadi mwezi. Watoto wengi walikuwa wanatangazwa makanisani au misikitini kuwa wamepotea. Walihifadhiwa kwenye vituo vya polisi. Sababu kubwa ilikuwa kupotea walipoufuata mdundiko.

Kuna mmoja akaniandikia kuwa hata Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) wakati huo, ilikuwa na kipindi chake maalum kiitwacho 'Kijaluba', kilichokuwa kiendeshwa na mtangazaji maarufu Abdallah Mlawa. Mbali na kutangaza sherehe mbalimbali zitakuwa wapi, kipindo hicho kilikuwa na kazi ya kutangaza majina ya baadhi ya watoto waliopotea. Asilimia 90 walikuwa wamepotea kwa kufuata mdundiko. Na waliokuwa wakienda kutoa matangazo hayo ni wazazi au walezi waliopotelewa na watoto hao.

Kwenye mbao za matangazo makanisani na hata vituo vya polisi walikuwa wakibandika picha za watoto waliopotea. Mama mmoja kwa sasa, ambaye alikuwa mtoto wa mmoja wa maofisa wa ngazi za juu wa Jeshi la Polisi wakati huo, akaniambia yeye wakati huo, akiwa binti mdogo sana, wakati huo walikuwa wanaishi Upanga alizolewa na mdundiko na kupotea.

Kumbuka sehemu hiyo walikuwa wanaishi watu wenye uwezo mkubwa sana au wenye nyadhifa kubwa serikalini. Yeye baba yake alikuwa ofisa mkubwa wa polisi. Akasema kwa sababu ni eneo tulivu na la watu wa hali ya juu, ilikuwa maajabu siku hiyo alipoona ngoma ya mdundiko inapita, hakujua imetoka wapi, lakini kwa sababu ni kitu kigeni na pia utoto, alichomoka ndani bila wazazi wake kujua na kujiunga na msafara wa watu waliokuwa kwenye ngoma hiyo.

"Nilicheza, nikaserebuka, wala sikujua tunaenda wapi. Ulipofika mwisho, sikujua nilipotokea wala nilipo. Kumbe tayari nilikuwa natafutwa na baba keshapiga 'radio call' kwenye vituo vyote vya polisi kunisaka. Watu waliniokota na kunipeleka kwenye kituo cha polisi Buguruni.

Ndipo nikagundua kuwa nipo Buguruni. Askari kwa sababu walikuwa wameshataarifiwa na baba, wakajua ndiye mimi mtoto wa bosi wao niliyepotea. wakanirudisha hadi nyumbani," anasema mama huyo ambaye kwa sasa ameolewa na ana familia yake, akisimulia tukio lililomtokea katikati ya miaka ya 1980.

Anakiri kuwa alipatikana siku hiyo hiyo kwa sababu ya cheo cha baba yake na alitumia 'radio call' kusambaza taarifa hiyo kwenye vituo vyote vya polisi. Kama isingekuwa hivyo, angeweza kukaa hata siku mbili tatu na zaidi kabla ya kujulikana alipo na kurejeshwa kwenye familia yake.

Huyo ni mmoja tu, lakini ni wengi sana wamekumbwa na kadhia hiyo. Si watoto wa kike au wa kiume. Nadhani kuna siku tunaweza kumpata mama wa wakati huo akiwa tayari ameolewa halafu akafuata mdundiko, akarejea na kukuta mumewe amerejea. Naye anaweza kutupa stori nini kilichomtokea.

**Kwa maoni piga au tuma ujumbe kupitia 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-2

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je, ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MWINGINE hadi leo ana makovu ya kuibiwa mtoto wake. Miaka mitatu iliyopita alimpata dada wa kazi kwa ajili ya kumlea mtoto wake wa mwaka mmoja, huku yeye akiwa ni mfanyakazi.

Anamuacha mtoto nyumbani na dada yeye akienda kazini. Siku isiyo ya jina hakumkuta mtoto wake, wala dada wa kazi. Hadi leo hajui walikotokomea. Huyu dada alikuwepo mahakamani. Moyoni hukumu hii ilimfurahisha sana, ingawa haikufuta machungu na majonzi aliyonayo.

Sio kinamama tu waliokuwa na masononeko na madada wa kazi, Hapo hapo mahakamani kuna baba mmoja yeye alikuwa na mfanyakazi wake wa ndani, akamtaka kimapenzi. Wakakubaliana vizuri. Alichofanya ni kumsafirisha mkewe kwenda kwao baada ya kupata msiba. Akaona nafasi si ndiyo hii.

Msichana kabadilika bwana. Akakataa. Baba akataka kumbaka. Msichana akafanikiwa kuchomoka na kukimbia. Akampigia simu mkewe na kumueleza kila kitu, huku akimwambia hawezi kurudi tena nyumbani kwake. Mke alivyorudi wala hakuwa na maneno mengi. Alichotaka ni talaka yake tu. Hakuliki hakulaliki mpaka baba wa watu katoa talaka. Hivi sasa hana hata mke. Mke hataki kurudi na hajaona bado. Huyu naye aliona sawa tu "Ndiyo wale wale tu." Alijikuta akitamka maneno hayo, ingawa ni sauti ya chini sana.

Hali ya mahakamani hapo ilikuwa ya tafrani, kila mmoja alisema lake na kila mmoja alikuwa na mtazamo wake.

Hayo yote hayakubadilisha ukweli. Ukweli wa kwamba, msichana wa miaka 18 tu, Tina Kauzeni kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa, baada ya mahakama kukubaliana na hoja zote za upande wa mashtaka kuwa alimuua mfanyabiashara Hafidh Chilambo kwa sumu iliyowekwa kwenye chakula. Chakula kilichopikwa na yeye mwenyewe. Akamtengea mezani. Akala na baada ya dakika kadhaa akasikia tumbo linamsokota, kabla ya kuanza kutokwa na mapovu.

Ushahidi wa daktari Thomas Mtuta na mfamasia Mwahija Chota ndiyo uliooneka-na kwa kiasi kikubwa kumuweka matatani zaidi Tina kupata hukumu hiyo.

Mlio wa karandinga ulisikika. Tayari lilianza kuondoka likimpeleka msichana huyo kupata adhabu yake inayomstahiki.

Minong'ono ikaanza pale pale mahakamani kuwa Tina aliahidiwa na baadhi ya wafanyabiashara kiasi kikubwa cha pesa ili amuue Chilambo.

Ikatajwa kuwa sababu marehemu aliwadhulumu wenzake pesa nyingi, baada ya kufanikisha kufanya biashara moja ya magendo iliyowapatia pesa nyingi.

"Jamaa hawakutaka kumuua kwa risasi kwa sababu alijua itajulikana kama ni wao. Wakamtumia msichana huyu mdogo kwa kumlipa kiasi kidogo tu cha pesa, lakini kwake kikubwa ili amuwekee sumu kwenye chakula afe. Walichotaka ni kwamba huyu msichana ndiyo aonekane ameua na sio wao," jamaa mmoja alimnong'oneza mwenzake nje ya mahakama hiyo, baada ya kila mmoja kuanza kutawanyika.

Eddy Kamal, mmoja wa wapelelezi mahiri nchini Tanzania alikuwepo kortini hapo kwa sababu zake binafsi.

Alikwenda kwenye ofisi ya rafiki wake ambaye ni wakili. Baada ya kumaliza kilichompeleka, aligundua kuwa kuna kesi yenye mvuto kwa sababu ina watu wengi mno.

Akaambiwa ni siku ya hukumu ya msichana ambaye anatuhumiwa kwa mauaji ya bosi wake. Kwa kawaida ni mdadisi. Akaamua kwenda kuisikiliza.

Aliisikia hukumu hadi mwisho. Kwa bahati mbaya sana hakujua mlolongo mzima wa kesi jinsi ulivyoendeshwa hadi mwisho.

Naye pia aliridhika na jinsi Jaji alivyohukumu kutokana na ushahidi ulivyotolewa upande wa mashtaka. Ni kweli kabisa kama ni hivyo msichana alistahili adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Hata hivyo, kilio cha msichana yule na mwanamke mwingine aliyemwita shangazi yake vilimfanya amuonee huruma. Hakuwa na la kufanya. Nje ya mahakama ndipo alipokutana na uvumi mwingi juu ya kesi hiyo.

Kwanza kabisa wapo waliosema kuwa msichana alimuua bosi wake kwa sababu alikuwa hajalipwa mshahara kwa muda wa miezi sita.

Uvumi mwingine ni kwamba alipokea kitita kikubwa cha pesa kutoka kwa wafanyabiashara ambao walitaka kumpeleka ahera kwa sababu aliwadhulumu pesa zao.

Hakujua ukweli ni upi. Akabaki njia panda. Hata hivyo, akajiambia kuwa haiwezekani mfanyabiashara kama Chilambo ashindwe kumlipa msichana kama yule mshahara wake.

"Inawezekana alikuwa anatoa anampa mkewe, halafu hampi mwenyewe kama ilivyo kwa baadhi ya wanawake wanavyofanya." Alijiambia.

Kitu ambacho alichogundua Eddy ni kwamba wakati wa kesi ile, waliokuwa watu upande wa mashtaka walikuwa ni wenye uwezo mkubwa, vyeo na walikuja kwa magari. Hao ni ndugu na jamaa wa pande zote za marehemu na mkewe pia, lakini upande wa utetezi kwanza kabisa walikuwa wachache. Pili walikuwa ni watu wa kawaida na vipato vidogo. Hii pekee ilimfanya naye kuingiwa na imani kama binadamu. Kabla ya kuingia kwenye gari lake alianza kuangalia huku na huko ili amuone yule mama aliyekuwa akilia sana pindi hukumu ilipotoka.


Alimuona kwa mbali akiwa na wale wale waliokuwa nao. Mtu mmoja mzima na msichana ambao walikuwa na kazi ya kubembeleza.

Njia waliokuwa wanatembea ilikuwa ni kando ya barabara, hivyo aliona bora aingie kwenye gari yake na atasimama akiwafikia. Akafanya hivyo.

"Habari zenu." Alisalimu baada ya kushusha kioo cha gari lake.

Aliowasalimu walisita kidogo. Lakini msichana akajibu nzuri shikamoo.

"Marahaba, mnaweza kupanda niwasogeze mbele?"




**"Poleni sana wazee wangu kwa tukio lile. Najua mmeumia sana, lakini kwa sasa mnatakiwa mrudi nyumbani kwa usalama na mapema zaidi. Mimi ni wakili kwenye mahakama hii na nimeona yote waliotokea, nimeona nijitoleaa tu niwarudishe nyumbani, ingawa na mimi nakwenda kwangu."**

Msichana aliwatazama aliokuwa nao, ambao walionekana ni kama bado wana msongo wa mawazo na hakutaka kufanya hivyo, ama walikuwa na hofu.

Eddy alipaki gari pembeni, akateremka. Akawafuata.

"Poleni sana wazee wangu kwa tukio lile. Najua mmeumia sana, lakini kwa sasa mnatakiwa mrudi nyumbani kwa usalama na mapema zaidi. Mimi ni wakili kwenye mahakama hii na nimeona yote waliotokea, nimeona nijitoleaa tu niwarudishe nyumbani, ingawa na mimi nakwenda kwangu." Aliwaondoa hofu.

"Kwani wewe unakwenda wapi." Sauti ya mzee ilisikika kwa mara ya kwanza akiuliza.

"Kwanza nataka niwapeleke nyinyi nyumbani, halafu mtajua mimi nakwenda wapi."

"Sisi tunaishi Tandale kwa Mtogole." alijibu. "Twendeni."

Mzee alimgeuka mkewe na kumsihi waingie kwenye gari. Msichana yeye alionekana yuko tayari tangu mwanzo. Tatizo lilikuwa na wazee wake.

Baada ya kimya cha dakika 10, Eddy aliitafuna lami. Aliamua kuvunja ukimya. "Mzee huyu mama ni mkeo?"

"Ndiyo ni mke wangu."

"Na huyu binti yako?"

"Sawa kabisa."

"Aliyehukumiwa na huyu nani mkubwa?"

"Hilo swali anayeweza kujibu ni mke wangu."

"Lakini naona kama hayupo vizuri kabisa." "Atajitahidi, eti mama Mwasi, umesikia swali la huyu kijana?"

"Baba nikwambie tu, yule siyo mwanangu wa kumzaa, ndiyo maana kama ulikuwepo mahakamani ulisikia akiniita shangazi."

"Ni mtoto wa kaka yako?"

"Hapana, yule alikuwa mfanyakazi wangu. Wakati anatoka kwao Mpanda, alipofika mjini alifikia kwangu. Kwa historia yake ni kwamba baba na mama yake walifariki zamani, akiwa mdogo. Kusema kweli jambo hilo lilinifanya kuishi naye sio kama mfanyakazi, bali ni kama binti yangu wa kumzaa na hata kazi kwa marehemu Chilambo aliipata akiwa kwangu na alitoka kwangu. Kwanza nilikataa kabisa kumruhusu, roho yangu ilikuwa nyeusii, leo hii Tina anakwenda kunyongwa, siamini." mama Mwasi akaanza kulia tena.

**INAENDELEA JUMAPILI**



## GALATONE WALIKUROGA? HAWAKUWEZI

KUMBE msanii Galatone hakuacha muziki kwa amri yake. Msikie mwenyewe anavyosema.

"Umaarufu nilishaupata, lakini nikapumzika muziki. Nikawaambia kichwa changu kimechoka. Niliona rahisi tu. Kumbe hujui tu inawezekana kabisa nilipigwa bomu moja zito. Unapigwa bomu jasho linakutoka. Sasa narudi upya. Wala sitotumia nguvu sana kwa sababu kama umaarufu nilishaupata," alisema msanii huyo ambaye alishatoa ngoma zilizobamba kama 'Ntajipitisha', 'Samaki', 'Sina Mali', 'Mshenga', 'Sokomoko' na nyingine nyingi.

Kuhusu kurogwa tena kama akirejea, alisema kwa sasa anasali sana. "Kwa sasa nimerudi nikiwa na imani na Mungu. Nasali sana. Mabomu yao wakiyatuma yatarudi yalikotoka," alisema msanii huyo ambaye jina lake halisi ni Hemed Sadallah.

Akizungumzia kama anaweza kuendana na msanii wa kisasa, alisema kila mmoja anafanya muziki wake na mashabiki wake.

"Kina Mr Blue sisi tuliwasikia tangu tuko darasa la pili A, lakini hadi leo wapo, wanaendelea na muziki, wana mashabiki wao pia," alisema. Kilichobaki kwa mashabiki ni kusubiri ngoma mpya tu ya Galatone.



# GIGY

## ANUNUA UGOMVI WA KIBA, SHILOLE

KILA mmoja anajua kinachoendelea mitandaoni kati ya Alikiba na Shilole baada ya Kiba kusema hakumualika Shilole kwenye uzinduzi wa albamu yake.

Shilole hakukaa kimya alikuja juu na kuhoji kwanini Alikiba anasema hivyo?

Mmoja wa mastaa wa Bongo Fleva, Gigy Money, hajakaa kimya amekuja mitandaoni na kutoa maoni yake kuhusu hilo.

"Shilole waache, wala usijali wewe ni staa, ndiyo maana wanakuzungumzia. Mimi hapa nilipo ni timu Shishi, nakupenda Shishi. Japo wanasema hujui kingereza, lakini mbona hata mimi sijui, lakini tunatrendi kila siku. Shishi ndiyo msanii wa kike mwenye pesa kwa sasa kuliko wengine wote kwa sababu ana biashara zake za chakula. Hata mimi simfikii. Jamani kwani mtu angekaa kimya ingekuwaje?

Kupitia Insta yake ameandika kuwa Shilole baada ya kuambiwa maneno yale kuwa alivamia sherehe za uzinduzi aliandika.

" Hapana jamani, kila siku nakosewa nikitaka kuongea washauri wangu wanasema nikae kimya. Hili nimekosewa sana sana na siwezi kukaa kimya, sasa mnanionea.

Haikuwa na haja kwenda redio na kusema "sijamualika" ili mimi nionekane nilivamia tu shughuli , sijapenda.

Kwa ufupi, sikwenda kwenye shughuli kama mvamizi. Nilialikwa.

Shughuli ile ya ovyo ovyo na kupoa kama uji wa mgonjwa, ilihitaji uwepo wangu, 'yes'. Niliwasaidia kuchangamsha.'

Haya ni baadhi ya maneno aliyoyaandika Shilole akimjibu Kiba.

Lakini kinachoshangaza na kushtua watu ni kwamba wakati wanatupiana maneno, muda huo huo, Shilole anatoa ngoma yake mpya aliyoiita 'Amsha Popo'.

Ngoma hiyo imeachiwa Ijumaa, hivyo baadhi ya mashabiki wanakwenda mbali sana na kusema, huenda 'bifu' hilo ni la kutengeneza kwa ajili ya kuipa kiki ngoma hiyo ambayo ipo kwa mfumo wa 'audio'.



## Naira unadhani staa hakamatwi?

MSANII nyota wa muziki kutoka Nigeria, Naira Marley, amepanda kizimbani kujitetea mashtaka yanayomkabili ya matumizi mabaya ya mitandao.

Naira ameonekana wiki hii akiwa na makaratasi ya ushahidi baada ya shauri kufunguliwa mahakamani.

Amesema katika ushahidi wake ana jumbe fupi 977 na mazungumzo ya vikundi 1,433 katika simu yake baada ya kukamatwa mwaka 2019 kwa tuhuma ya kutoa kashfa kwa wasanii wengine.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RODGERS ANUKIA UNITED**

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers anapewa nafasi kubwa ya kutangazwa kuwa mrithi, Ole Gunnar Solskjaer katika kikosi cha Manchester United. **(ESPN)**

**SALAH, LIVERPOOL SAFI**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mweye umri wa miaka 29, atakubali kuongeza mkataba mpya kabla ya dirisha la uhamisho la Januari halijafika. **(Football Insider)**

**RONALDO NA URENO 2026**

FOWADI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, anataka kuichezea Timu ya Taifa ya Ureno kwenye fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2026. **(Sun)**

**HAZARD APATA BARAKA**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti atamruhusu fowadi wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 30 kuondoka klabuni hapo kama anataka. **(Marca)**

**XAVI YUKO TAYARI**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anaamini gwiji wa Barcelona, Xavi yupo tayari kuchukua mikoba ya kuinoa klabu hiyo ya Hispania. **(Goal)**

**COMAN ANUKIA BARCA**

XAVI atajaribu kumsajili winga wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 25 kama atakuwa kocha mpya wa Barcelona. **(Sport)**

**ARTETA AIKATAA BARCA**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amekataa kuhusishwa na mpango wa kutakiwa kuwa kocha mpya wa Barcelona, klabu ambayo ilimlea katika mchezo**. (Sky Sports)**

**NEWCASTLE YAMFUATA LINGARD**

NEWCASTLE inajipanga kumsajili nyota wa Manchester United, Jesse Lingard. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua katika klabu hiyo hapo Januari. **(Sun)**

**RUDIGER NJIA MOJA**

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua Liverpool. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye ni raia wa Ujerumani utamalizika mwishoni mwa msimu huu. **(Express)**


**MARTINEZ KUMRITHI LLORIS**

GOLIKIPA wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Argentina, Emiliano Martinez (29), anapewa nafasi kubwa ya kutua Tottenham Hotspur ili kuchukua mikoba ya Hugo Lloris (34), ambaye anaondoka mwishoni mwa msimu huu. **(Independent)**

**TERRY NA NEWCASTLE**

MLINZI wa zamani wa Timu ya Taifa ya England na Chelsea, John Terry, anatajwa kuwania nafasi ya kuwa kocha mpya wa Newcastle United. **(Mirror)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAKATAA KUMUUZA POGBA

**Ni katika dirisha dogo la Januari licha ya mkataba wa kiungo huyo kuelekea...**

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United haitamuuza Paul Pogba ifikapo Januari mwakani licha ya Mfaransa huyo atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa gazeti la The Telegraph.

Majaliwa ya Pogba katika kikosi cha Manchester United yamebaki na sintofahamu kuhusu kuongeza mkataba mpya na klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hadi sasa hajakubali kusaini mkataba mpya na klabu hiyo na kumekuwa na ripoti anataka kuondoka.

Pogba alianza msimu huu vizuri na United, lakini Jumapili alitolewa nje kwa kadi nyekundu wakati United wakichezea kichapo cha mabao 5-0 kutoka kwa Liverpool.

United walimsajili Pogba kwa pauni milioni 89 mwaka 2016 akitokea Juventus, ambayo pia inahusishwa kumtaka tena.

Real Madrid na Paris Saint-Germain pia ni miongoni mwa timu ambazo kiungo huyo anahusishwa nazo.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Timu ya Taifa ya Ufarasa aliripotiwa kukwaruzana na kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer ingawa yeye mwenyewe alikanusha madai hayo.

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME
ROMA
2.27 | 3.49 | 2.99
AC MILAN
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ERIKSEN AWEKWA SOKONI INTER MILAN



**MILAN, Italia**

KLABU ya Inter Milan imetangaza kumweka sokoni kiungo mshambuliaji wake, Christian Eriksen, kutokana na sheria za Ligi Kuu Italia, Serie A, zinazomzuia kucheza mashindano yeyote kwa sababu ya kuwekewa kifaa cha kusaidia mapigo ya moyo.

Eriksen ambaye alianguka kwenye mchezo wa euro 2020 dhidi ya Finland na kuwahishwa hospitali kutokana na kupatiwa matibabu ya kuweka kifaa maalum ambacho kinasimamia mwenendo wa mapigo ya moyo wake.

Kwa mujibu wa sheria za Ligi Kuu Italia, mchezaji yoyote ambaye amewekewa kifaa cha kusaidia mapigo ya moyo haruhusiwi kucheza kwenye mashindano yoyote kwenye nchi hiyo.

Taarifa iliyotolewa na Inter Milan imesema, "tukirejea haki ya usajili wa Eriksen, kutokana na tatizo lake lililotokea kwenye mashindano ya Ulaya, anazuiliwa na mamlaka ya utabibu kujihusisha na michezo yote kwa sasa nchini Italia.

"Ingawa kwa hali aliyokuwa nayo anaweza kuruhusiwa kucheza sehemu nyingine na anaweza kufanikiwa katika nchi nyingine na kuendelea na kazi yake kama kawaida."

Eriksen ameichezea Inter Milan michezo 60 na kuifungia mabao nane, pia amekuwa mmoja wa wachezaji walioisaidia Inter kutwaa ubingwa wa Serie A msimu uliopita ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha misimu 10.



# Barca kumpa mikoba Xavi

**BARCELOBA, Hispania**

BARCELONA wapo kwenye mazungumzo na Xavi Hernández ili kumfanya kuwa kocha mkuu wa timu hiyo baada ya kumfukuza, Ronald Koeman.

Kiungo huyo wa zamani wa Barcelona ambaye kwa sasa anafundisha Al Sadd ya nchini Qatar anataka kurejea kwenye viunga vya Camp Nou na sasa mazungumzo yanafanyika ya kuvunja mkataba na klabu yake hiyo anayoifanyia kazi.

Bodi ya Barcelona imekuwa ikiwasiliana na Xavi kuhusu kurithi mikoba ya Koeman kwa wiki kadhaa, na watafanya uamuzi ya kumpa mikoba ya Koeman kabla ya mchezo wao leo Jumapili dhidi ya Alaves.

Xavi ambaye amekulia kwenye akademi ya La Masia, amecheza michezo 767 na kwa mara ya kwanza alitambulishwa na Luis Van Gaal mwaka 1991 kwenye timu ya vijana kabla ya kuingia rasmi kwenye timu ya wakubwa mwaka 1998.

Xavi amecheza kwa mafanikio akiwa na Barcelona ambapo alichukua mataji 27 na aliachana nayo mwaka 2015.

Alikwenda Qatar kuichezea Al Sadd katika mechi 82 na kufunga mabao 21 na kutundika daluga na kuchukua mikoba ya kuwa kocha mkuu.

LIVE IN PLAY

# TANZANITE YAANZA VYEMA CECAFA U-20

**Na Mwandishi Wetu, UGANDA**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana ya wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), imeanza vyema mashindano ya kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati kwa kufunga Eritrea bao 1-0 kwenye mechi iliyochezwa jana asubuhi katika mji wa Njeru nchini hapa.

Mechi hiyo iliyokuwa na ushindani, kila timu ilijaribu mashambulizi mbalimbali, lakini ilishuhudiwa dakika 45 za kwanza kila upande ukishindwa kutikisa nyavu za mwenzake.

Bao pekee katika mchezo huo ambalo liliipa Tanzanite Queens pointi tatu muhimu lilifungwa na Clara Luvanga dakika ya 90.

Kikosi hicho cha Tanzanite Queens kitashuka tena dimbani kesho kuwakabili yosso wenzao kutoka Burundi kuanzia saa 10:00 jioni wakati mechi ya asubuhi itakuwa ni kati ya Uganda dhidi ya Djibouti.

Mechi nyingine ya mashindano hayo yanayoshirikisha nchi sita kati ya 13 wanachama wa Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), itakuwa ni kati ya 'Wanandugu' Ethiopia dhidi ya Eritrea.

Mashindano hayo yanayochezwa kwa mkondo mmoja yanatarajiwa kumalizika Novemba 9, mwaka huu na timu itakayokuwa na pointi nyingi itatangazwa mabingwa.



Kiungo mkabaji wa Tanzanite Queens, Irene Kisisa (kulia), akijaribu kumtoka mchezaji wa Eritrea katika mechi ya mashindano ya Kombe la CECAFA U-20 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Njeru, Uganda jana. Tanzanite Queens ilishinda bao 1-0. **PICHA: TFF**

# Mafunzo yaipania Machomane Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa Ngao ya Jamii mwaka huu, Mafunzo wanatarajia kuvaana na Machomane katika mechi ya Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Mau visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Abdallah Bakari 'Edo' alisema msimu huu unatarajiwa kuwa na utakuwa na ushindani kwa sababu kila timu imejiandaa vizuri kuwania taji la ligi hiyo.

Edo alisema kikosi chake kimejiandaa kuendelea na mapambano kama walivyofanya katika msimu uliopita kwa kuhamasisha wachezaji wao ndani na nje ya uwanja.

> **"Tutaendelea na mapambano yale yale, tunajua msimu huu utakuwa ni wenye vita zaidi kutokana na kila timu kuonyesha nia ya kutaka ubingwa," alisema Edo.**

Alisema katika mchezo wao dhidi ya Machomane ya Pemba wamejipanga kutoka na ushindi ambao utaendeleza hamasa waliyoanza nayo.

Aliongeza wataingia uwanjani kuwakabili Machomane kwa nidhamu na kila mchezaji anatakiwa kutekeleza vyema majukumu yake.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA

PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 31 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 2818 | Sparta Rotterdam vs Feyenoord | 5.49 | 4.41 | 1.49 |
| 14:30 | 1930 | Inter vs Udinese | 1.35 | 5.19 | 7.98 |
| 15:00 | 3067 | Angers vs Nice | 2.84 | 3.29 | 2.45 |
| 16:00 | 1982 | Fuenlabrada vs Girona | 2.87 | 3.02 | 2.53 |
| 16:00 | 2357 | Randers vs Midtjylland | 3.30 | 3.35 | 2.11 |
| 16:00 | 4258 | Lamia vs Atromitos | 2.34 | 3.01 | 3.16 |
| 16:00 | 5043 | Nordsjalland vs Aalborg | 2.85 | 3.49 | 2.29 |
| 16:00 | 5069 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.53 | 2.93 | 3.08 |
| 17:00 | 1248 | Bordeaux vs Reims | 2.47 | 3.19 | 2.89 |
| 17:00 | 3253 | Strasbourg vs Lorient | 1.94 | 3.48 | 3.83 |
| 17:00 | 3405 | Helsingborg vs IK Brage | 1.68 | 3.91 | 4.82 |
| 17:00 | 3538 | Montpellier vs Nantes | 2.32 | 3.39 | 2.94 |
| 17:00 | 3750 | Norwich City vs Leeds | 3.35 | 3.50 | 2.10 |
| 17:00 | 4416 | Fiorentina vs Spezia | 1.55 | 4.31 | 5.41 |
| 17:00 | 4480 | Sassuolo vs Empoli | 1.77 | 4.10 | 4.00 |
| 17:00 | 4598 | Troyes vs Rennes | 3.74 | 3.44 | 1.97 |
| 17:00 | 5311 | Genoa vs Venezia | 2.02 | 3.45 | 3.65 |
| 17:00 | 5580 | Norrkoping vs Elfsborg | 2.39 | 3.37 | 2.60 |
| 17:30 | 5912 | Augsburg vs Stuttgart | 2.88 | 3.28 | 2.42 |
| 18:00 | 3394 | Copenhagen vs Vejle BK | 1.29 | 5.34 | 9.10 |
| 18:15 | 1046 | Panathinaikos vs OFI Crete | 1.59 | 3.59 | 5.90 |
| 18:15 | 4894 | Atletico Madrid vs Betis | 1.58 | 3.94 | 5.79 |
| 18:45 | 3866 | Waalwick vs Cambuur | 2.46 | 3.50 | 2.61 |
| 19:00 | 1492 | Genclerbirligi vs Istanbulspor | 2.06 | 3.38 | 3.14 |
| 19:00 | 1614 | Brest vs Monaco | 4.37 | 3.78 | 1.75 |
| 19:00 | 5180 | Denizlispor vs Kocaelispor | 2.85 | 3.34 | 2.22 |
| 19:00 | 5999 | Galatasaray vs Gaziantep BB | 1.44 | 4.45 | 6.33 |
| 19:30 | 1774 | Orebro SK vs Djurgardens IF | 6.72 | 4.70 | 1.35 |
| 19:30 | 3733 | Aston Villa vs West Ham | 2.80 | 3.40 | 2.45 |
| 20:00 | 1263 | Viking vs Sarpsborg | 1.71 | 3.95 | 4.24 |
| 20:00 | 1620 | Salernitana vs Napoli | 8.19 | 5.39 | 1.33 |
| 20:00 | 2707 | Viborg FF vs Brondby | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 20:00 | 4021 | Bodo Glimt vs Sandefjord | 1.25 | 6.11 | 8.87 |
| 20:15 | 5521 | Valladolid vs Eibar | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 20:30 | 2590 | Anderlecht vs OH Leuven | 1.28 | 5.72 | 8.29 |
| 20:30 | 3631 | AEK Athens vs Aris Salonica | 1.85 | 3.36 | 4.25 |
| 20:30 | 5112 | Getafe vs Espanyol | 2.33 | 3.05 | 3.30 |
| 20:30 | 5540 | Partizan vs Cukaricki St | 1.17 | 6.16 | 12.52 |
| 21:00 | 2322 | Belenenses vs Santa Clara | 2.95 | 3.05 | 2.45 |
| 21:00 | 5000 | Al Ahly Cairo vs National Bank | 1.22 | 5.93 | 11.87 |
| 21:15 | 5905 | Hapoel Tel Aviv vs Bnei Sakhnin | 1.53 | 3.60 | 5.96 |
| 22:00 | 3270 | Valerenga vs Brann | 1.90 | 3.75 | 3.56 |
| 22:00 | 4025 | Sonderjyske vs Silkeborg | 2.86 | 3.35 | 2.34 |
| 22:00 | 5703 | GO Ahead Eagles vs Fortuna Sittard | 1.83 | 3.64 | 3.88 |
| 22:30 | 4312 | Zaragoza vs Mirandes | 1.74 | 3.45 | 4.63 |
| 22:45 | 1093 | Clermont Foot vs Marseille | 2.88 | 3.48 | 2.32 |
| 22:45 | 4823 | Roma vs AC Milan | 2.27 | 3.49 | 2.99 |
| 23:00 | 1027 | Real Sociedad vs Athletic Bilbao | 2.11 | 3.20 | 3.65 |
| 23:00 | 3116 | KAA Gent vs Union Saint Gilloise | 2.33 | 3.39 | 2.85 |
| 23:30 | 4901 | Famalicao vs FC Vizela | 2.02 | 3.35 | 3.55 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Oktoba 31, 2021
Nipashe



United yakataa kumuuza Pogba

HABARI UK 21

## Yanga yafunguka mwendo wa dozi

**Na Saada Akida**

IMEBAINIKA! KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amewe-ka wazi tatizo la kikosi chao kupata ushindi 'kiduchu' katika mechi za Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara zinazoendelea kuwa ni ubinafsi wa washambuliaji wa timu hiyo na tayari wameshalipatia ufumbuzi.

Kabla ya mechi ya jana usiku, Yanga ilikuwa imecheza mechi tatu na imefunga mabao manne, haijaruhusu nyavu zake kutingishwa.

Kaze aliliambia gazeti hili timu hiyo inatengeneza nafasi nyingi za kufunga lakini wanazipoteza kwa sababu kila mmoja anahitaji kufunga hata pale isipowezekana.

Kocha huyo alisema benchi la ufundi limejitahidi kuwaeleza washambuliaji wao namna wanavyotakiwa kufanya uamuzi ili wapate ushindi mnono katika kila mechi watakayocheza.

"Mechi zilizopita tulifanikiwa kutengeneza nafasi nyingi, na ninaimani washambuliaji wetu wako vizuri kwa asilimia 100, kinachowaangusha ni kuwa wabinafsi. Wakifuata tunachowaambia tutashinda kwa mabao mengi," Kaze alisema.

Aliongeza endapo kila mchezaji ataonyesha ushirikiano mzuri kwa mwenzake, suala la kufunga halitakuwa tena 'pasua kichwa' kwenye kikosi cha Yanga.

"Tunahitaji kupambana na hali hiyo, kazi kubwa inaanza kwa viungo na mipira kufika kwa washambuliaji na kuhakikisha wachezaji wote wanacheza kwa ushirikiano mkubwa," alisema Kaze.

Baada ya mechi ya jana usiku dhidi ya Azam FC, Yanga itabakia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini kuwasubiri 'Maafande' wa Ruvu Shooting kwa ajili ya mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa keshokutwa.



Mshambuliaji wa Arsenal, Emile Smith Rowe (katikati), akifunga bao katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Leicester City iliyochezwa kwenye Uwanja wa King Power jana. Arsenal ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, COASTAL MECHI YA REKODI

### ●●●Wagosi wa Kaya wasema 'uteja' sasa basi, wajipanga...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi, Simba, wanatarajia kuwakaribisha Coastal Union kutoka Tanga katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Simba itashuka uwanjani leo ikiwa na nguvu mpya katika bechi ya ufundi baada ya kocha wake msaidizi, Selemani Matola, kurejea kikosini akitokea kwenye kozi ya ukocha ngazi ya leseni A, inayotambulika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Wekundu wa Msimbazi watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 7-0 walioupata ugenini na waliporejeana waliondoka na ushindi wa magoli 2-0.

Kuelekea mchezo wa leo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Thierry Hitimana, alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa yenye ushindani na itakayovutia kutokana na uchezaji wa aina ya timu hizo mbili zinazokutana.

Hitimana alisema Simba iko tayari kwa ajili ya kupambana na kupata ushindi mwingine huku vijana wake wakiwa imara, tayari kiufundi na kisaikolojia.

"Tumefanya maandalizi vizuri, tunahitaji kupata ushindi, tunakubali na ni ukweli hatujaanza vizuri msimu huu. Tumeanza kwenye hali ngumu. Lakini tumekaa na kukumbushana lazima tuhakikishe tunarejea kwenye hali yetu ya kawaida iliyozoeleka. Tukae sawa na kuutetea ubingwa wetu," alisema Hitimana.

Aliongeza wachezaji wake wanaendelea kuimarika kadri mechi zinavyokwenda na kila mmoja anatakiwa kutekeleza vyema majukumu atakayopewa.

Naye Matola alisema Simba imejiandaa kutuliza 'presha' ya wanachama na mashabiki wao kwa kupata ushindi kama ilivyokuwa kwenye mechi iliyopita dhidi ya Polisi Tanzania.

"Tulicheza kwa presha kubwa sana katika mechi iliyopita, hasa kwenye safu ya ushambuliaji, tutahakikisha mechi hii tunapata ushindi wa mabao mengi zaidi ya mechi zilizopita za msimu huu," alisema Matola.

Aliwataja wachezaji watakaoendelea kuwakosa ni Taddeo Lwanga na Ousmane Sakho ambao bado hawajakuwa fiti kukabiliana na mikikimikiki ya ligi hiyo itakayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Salim Waziri, alisema wamejiandaa vizuri na wamejipanga kuhakikisha 'wanafuta uteja' dhidi ya mabingwa hao watetezi kwa kuondoka na ushindi.

"Tunakwenda kutafuta matokeo mazuri. Tumekuwa tukipoteza mechi dhidi ya Simba, ila msimu huu tumejiandaa vizuri na wachezaji wote wako fiti kuhakikisha tunapata pointi tatu muhimu katika mchezo wetu huo," alisema Waziri.

Aliongeza wamekuja Dar es Salaam kutafuta pointi tatu na wanamatumaini makubwa kutokana na maboresho yaliyofanywa katika kikosi chao pamoja na benchi la ufundi.

Hija Ugando, Nahodha wa Coastal Union, alisema anatumia faida ya kuitumikia Simba kwa kuwajenga wachezaji wenzake kutokuwa na presha yoyote kuelekea mchezo huo wa raundi ya nne.

"Tunakutana na timu kubwa, tumejiandaa vizuri na tunawaheshimu Simba, tunatambua ni timu ambayo ina wachezaji wazuri ila tunaenda uwanjani kupambana nao kwa kila hali ili kupata matokeo mazuri," alisema Ugando.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Mbeya Kwanza kuwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.

9 770856 541002 >